# MAISHA MAPYA NDANI YA KRISTO



**Toleo la 1**

---

**Hatua za msingi katika maisha ya Mkristo**

Hili ni toleo la kwanza la Kiswahili la Maisha mapya ndani ya Kristo. Toleo hili lilitolewa kwa mara ya kwanza kabisa kwa Kiispaniola kama NUEVA VIDA EN CRISTO. Kusudi lake ni kukupa msingi imara katika maisha yako ya Kikristo.

Utakapomaliza toleo la 1, endelea na toleo la 2.

Kwa maelezo zaidi tuandikie barua pepe: **info@nuevavidaencristo.org**

Unaweza pia kupata nakala ya kitabu hiki na vitabu vingine kupitia mtandao huu:
**www.NewLifeDiscipleship.com**

Nakala hii ipo kwenye mfumo wa PDF na itahitaji Adobe Acrobat Reader ili kukisoma.

Matoleo yote yanapatikana pia katika Kiswahili, Kiengereza, Kifaransa, Kispaniola, Kireno. Matoleo mengine yanapatikana katika lugha zingine kama Kinyarwanda.

Umeruhusiwa kufanya nakala ya nyenzo hii kwa masharti kwamba unaelezea chanzo ya awali na kutofanya mabadiliko au nyongeza kwa maudhui yake.

Copyrighted 1993 © Mark Robinson
Toleo la kwanza la Kingereza 2002.
Camino Global
8625 La Prada Dr., Dallas, TX 75228 USA

20 Februari 2015

# YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| Mwongozo kwa Mwalimu | | 3 |
| Utangulizi kwa maisha ya Mkristo | | 5 |
| Hatua ya 1 | Kuokoka! | 7 |
| Hatua ya 2 | Salama! | 8 |
| Hatua ya 3 | Ushindi! | 10 |
| Hatua ya 4 | Bwana wa Vyote | 12 |
| Hatua ya 5 | Kuishi katika Roho | 14 |
| Hatua ya 6 | Mungu husema Nami | 16 |
| Hatua ya 7 | Kuzungumza na Mungu | 18 |
| Hatua ya 8 | Kukutana na Mungu kila siku | 20 |
| Hatua ya 9 | Kanisa langu | 23 |
| Hatua ya 10 | Kushuhudia! | 25 |
| Hatua ya 11 | Ubatizo na meza ya Bwana | 27 |
| Hatua ya 12 | Jamaa | 29 |
| Hatua ya 13 | Kumfuata Yesu | 31 |
| Maelezo ya ziada | | 33 |



# MWONGOZO KWA MWALIM

1. Tunakupongeza kwa kukubali changamoto la kuwafanya waumini wapya kuwa wanafunzi kwa kutumia kitabu cha "Maisha Mapya Katika Kristo" kama mwongozo wako. Matokeo ya masomo haya yanaweza kuzaa tunda la milele.

2. Biblia iwe mamlaka yako katika kujibu maswali yote wakati wote. Mwanafunzi ni lazima atafute vifungu vya Biblia yeye mwenyewe, na kujaribu kujibu maswali kufuatana na jinsi Biblia inavyosema. Waumini wengine wapya wanahitaji kukabilishwa vyema jinsi ya kutafuta kifungu katika Biblia.

3. Kitabu hiki kinaweza kutumika kwa njia nyingi. Wakati mwingi, unaweza kusoma somo moja kwa Juma, huku ukiwatia moyo wanafunzi kufanya kazi zote katika kila somo.

4. Jaribu kufanya kipindi chako kisiwe cha muda mrefu sana.

5. Watie moyo wanafunzi kujibu maswali kwa kutumia maneno yao wenyewe, wakiepuka kunakili moja kwa moja kutoka kwenye Biblia.Hii itamsaidia mwanafunzi kuchanganua maana ya maandiko aliyojifunza.

6. Epuka kuhubiri. Tumia maswali ili uweze kugundua yale wanafunzi wanachoelewa na uweze kuwachochea kushiriki.

7. Jiandae vizuri wewe mwenyewe katika kila somo. Kama mwalimu, inakupasa kufahamu vifungu na mawazo makuu kwa kila kifungu. Unapojiandaa, ombea wanafunzi na moyo wako ili uwe tayari kwa somo.

8. Jaribu kufanya wanafunzi wafikiri juu ya matokeo ya masomo haya katika maisha yao. Wasaidie kuelewa matumizi kamili kwa vitendo.

   Maswali yaliyoko katika kisanduki pembeni yanakusudi la kufanya wanafunzi kuweka masomo hayo kwa vitendo katika maisha yao. Hivyo basi, yatumie.

9. Wasaidie wanafunzi waweze kuwa na tabia ya kuomba. Wafundishe kwa kuomba pamoja nao.

10. Ni muhimu kuelewa kwamba kufanya watu kuwa wanafunzi ni zaidi ya kujifunza masomo kumi na tatu katika kitabu cha 'MAISHA MAPYA KATIKA KRISTO.' Uanafunzi una maana ya mabadiliko katika maisha ya mwanafunzi.

    Hiki kitabu ni msaada wa kutanguliza tu. Mwanafunzi anahitaji kuendelea kusaidiwa kutafuta namna ya kubadili tabia yake, namna ya kufikiri, mwenendo wake, na kadhalika.

11. Ni muhimu sana mwanafunzi kujifunza jinsi ya kuenenda kwa kusoma Biblia kila siku, kuomba, na kuweka vifungu vya Biblia kichwani.

    Unapoanza kila somo, chukua muda wa kumkumbusha mwanafunzi wako kifungu cha kukariri katika somo lililopita na kupate kuwauliza jinsi wanavyoendelea katika kusoma Biblia kila siku.

12. Uwe makini katika kutambua yale Mungu anayafanya katika maisha ya mwanafunzi. Katika kila somo, chukua muda wa kujibu swali lolote ambalo mwanafunzi wako anakumbana nalo, na kusaidia iwapo ana swala linalotatiza maisha yake.

    Yakupasa ufahamu kwamba unaweza kukosa muda wa kujibu maswali yote katika kila somo. Ikiwa hivyo, chagua maswali yaliyo muhimu sana, ambayo yanaweza kujadiliwa.

## Karibu Katika Jamaa Ya Mungu

Ulianza maisha mapya ya ajabu pamoja na Kristo ulipomwamini. Lengo la kitabu hiki ni kukufanya uweze kujua Biblia isemavyo kuhusu maisha ya Mkristo. Kukua katika Kristo ni hatua kwa hatua. Kila siku tunapaswa kulishwa na kutembea pamoja na Kristo. Kadiri tutoavyo muda wetu kwa ajili ya ushirika wetu pamoja naye, ndivyo tutakavyopiga hatua hadi kukomaa.

## Muhtasari wa jinsi ya kutembea pamoja na Kristo


1. Soma Biblia kila siku ili kumjua Kristo vizuri.
2. Zungumza na Mungu kila siku kwa maombi.
3. Mruhusu Mungu atawale maisha yako, ukijisalimisha kwa mapenzi yake.
4. Zungumza na wengine kuhusu habari za Kristo.
5. Tafuta kuwa na ushirika na waumini wengine katika kanisa ambalo Kristo anahubiriwa.
6. Tafuta mwamini mmoja au wawili, ambao unaweza kuomba nao na kuwashirikisha mafanikio yako, na pia kushindwa kwako.
7. Onyesha kwa vitendo maisha yako mapya kwa kuonyesha upendo na shauku ya kuwajali wengine.


## Maisha inayotawaliwa na Kristo

Maisha ya Mkristo yanaweza kuwakilishwa na picha ya msalaba. Kristo ndiye kiini cha maisha yetu mapya. Tunaishi kwa kujisalimisha kwake.

Mstari ulio wima, unawakilisha ushirika wetu pamoja na Mungu kwa maombi na kwa kusoma Biblia.

Mstari wa mlalo unawakilisha ushirika wetu na watu wengine. Tunapaswa kutafuta ushirika na waumini wengine katika kanisa. Tunapashwa kuwaambia wale ambao hawajaamini habari za Kristo.






Hatua ya 1
# Kuokoka

Jibu KWELI (K) au SI KWELI (S)
_______ Kuokoka ni kuamini tu kwamba Mungu yupo.
_______ Dhambi inasababisha utengano kati ya Mungu na mwanadamu.
_______ Mimi nimeokolewa kwa kwenda kanisani na kufanya matendo mema.

## MAISHA YA KALE

1. Kutokana na Waefeso 2:1, Je hali yetu ilikuwaje kabla Kristo kutupa uzima wa milele? ______________________

2. Soma Warumi 3:23. Je hiyo ina maana kila mtu alitenda dhambi?
Ndiyo ❏ La ❏ Kama hivyo ndivyo ilivyo, Je hali yetu ilikuwaje kabla Kristo hajatuokoa? ______________________
______________________

3. Biblia inasema kwamba, tulikuwa tumekwisha hukumiwa. Je ni kwa nini? (Yohana3:18) ______________________
______________________

## KAZI YA MUNGU

4. Je katika Waefeso 2:4-5, Mungu ametajwa vipi? ______________________
______________________

5. Kwa mujibu wa kifungu hiki, Mungu amefanya nini kwa ajili yetu?
______________________

6. Soma Warumi 5:8, Je ni jinsi gani Mungu anaonyesha pendo lake kwetu? ______________________

7. Soma Waefeso 2:8-9. Mungu aliamua kwamba tusiokolewa kwa matendo yetu (kifungu cha 9). Je ni matendo gani mazuri ambayo watu wanayafanya ili wapate kuokolewa? ______________________
______________________

8. Tunaokolewa kwa ______________ kwa njia ya ___________ (Kifungu cha 8).

   Neema maana yake ni "zawadi ambayo hatukustahili kupata". Kwa maneno mengine ni kwamba Mungu alitupa wokovu wa bure, ingawa hatukustahili.

9. Je tumwamini nani ili tuweze kuwa watoto wa Mungu?
(Wagalatia 3:26) ______________________

### WAKATI WA KUAMUA

Kama umekwisha kumpokea Kristo kama Mwokozi wako, andika hapo chini tarehe uliyofanya huo uamuzi. (ikiwa unakumbuka)

______________________

Kama bado hujampokea, Je ungependa kufanya hivyo sasa?

Ndiyo ❏ Hapana ❏

Kama umemkubali hivi leo, basi andika tarehe ya leo hapo chini.

______________________

### HEBU FIKIRI

Hebu fikiri juu ya nyumbani kwako, kila mmoja, na kila kitu unachokipenda. Je ni jinsi gani dhambi zako zimewaathiri?

Fikiri juu ya maisha yako ya baadaye. Kama ungeliendelea na maisha yale ya zamani,ungelikumbana na hukumu ya Mungu. Soma Ufunuo 20:11-15 na utafakari juu yake, ukimshukuru Mungu kwa upendo wake mkuu.


Matendo yako yamebadilika sasa kwa kuwa uko ndani ya Kristo na umekuwa kiumbe kipya. Andika hapa chini baadhi ya mabadiliko ambayo umeona tangu Juma lililopita.

______________________
______________________
______________________
______________________

**KUWA IMARA**

Ni muhimu kutafuta tabia ambazo zitakusaidia kukua katika maisha mapya.

Kama vile mazoezi huimarisha mwili, kuna mazoezi katika masomo ya kiroho yanayoweza kukusaidia kukua katika Kristo.



Hayo mazoezi ni kama vile:
- Kuchunguza Biblia
- Maombi
- Kukariri vifungu vya Biblia

**Kando na kumaliza masomo haya, ni muhimu kusoma vifungu vya Biblia na kumwomba Mungu kila siku.**

**Wiki hii usome sura ya 1-7 katika kitabu cha Yohana, sura moja kwa siku.**

Muombe Mungu kabla hujaanza kusoma, uandae moyo wako kupokea yale Mungu atakayokuambia kupitia kwa Neno lake.

Baada ya kusoma kila sura, fanya tena maombi, zungumza na Mungu kuhusiana na kile ulichokisoma.

Kwa msaada wa Mungu, ninajitolea kusoma sura moja ya Biblia kila siku.

____________________
Tarehe

**Kariri Waefeso 2:8-9**

***"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu".***

Katika maelezo ya ziada #1 utapata kadi itakayo kusaidia

_

10. Eleza kwa maneno yako mwenyewe maana ya kuwa na imani katika Kristo. ____________________________________________

_

**MAISHA MAPYA**

11. Je Kristo alikuja kwa kusudi gani? (Yohana10:10) ________________

________________________________________________________

12. Je Mungu anampa nini mtu aliyempokea Kristo? (Yohana1:12)

________________________________________________________

13. Kwa mujibu wa Yohana 5:24, ni kitu gani kinachotokea wakati mtu anapompokea Kristo? ____________________________________

14. Je Mungu alituumba kwa kusudi gani kutokana na Waefeso 2:10

________________________________________________________

***Kumbuka kwamba hatukuokolewa kwa matendo yetu bali tumeokolewa ili tufanye matendo mazuri.***

15. Soma 2 Wakorintho 5:17.Kuwa "ndani ya Kristo" ina maana ya kumpokea Yeye kama Mwokozi. Hivyo kama mtu yu ndani ya Kristo' anafanyika kuwa nani? ____________________________________

16. Eleza kwa maneno yako mwenyewe maana ya kifungu kinachosema, "ya kale yamepita, tazama yamekuwa mapya." ________________

________________________________________________________

________________________________________________________

________________________________________________________

**KWA MUHTASARI**

Kwa maneno yako mwenyewe, eleza kwa kifupi kile umejifunza leo.

1. Je maisha yako yalikuwaje kabla ya kumpata Kristo? _________

________________________________________________

2. Je Kristo alifanya nini kwa ajili yako? ____________________


________________________________________________

________________________________________________

3. Je utaonyeshaje katika maisha yako ya kila siku maisha mapya ambayo Mungu amekupatia? ________________________________

________________________________________________

________________________________________________




# Hatua ya 2
# Salama!

Jibu KWELI (K) au SI KWELI (S)
______ Nina hakika sasa kwamba nimeokoka
______ Mungu anahitaji nifanye dhambi ili aonyeshe upendo wake kwa wingi.
______ Nikifanye dhambi alafu nife bila kutubu, bado nimeokoka.

**MUNGU AMENIPA ULIZI**

1. Soma Waruma 8:38-39. Mara tunapokuwa tumempokea Kristo, je kuna namna tunavyoweza kutenganishwa na upendo wa Mungu? _________
_______________________________________________

Soma **Yohana 10:27-29** na ujibu swali la 2 hadi 7

2. Ni kitu gani kilichotolewa kwa ajili yetu? (kif. 28)____________________
3. Ni nani anayetoa uzima wa milele? (kif. 28)________________________
4. Je kitu cha milele kinaweza kufikia mwisho? (kif.28)_________________

Kiarifa "toa" kipo katika wakati uliopo. Hii inamaanisha kwamba tayari tunao uzima wa milele. Uzima wa milele unaanza mara tu tunapompokea Kristo kama Mwokozi wa maisha yetu, bali sio tunapokufa.

5. Je ni wakati gani tutakapoangamia? (kif.28)________________________

Hi inaonyesha wazi wazi kwamba uzima wa milele hauna mwisho.

6. Je kuna mtu au kitu chochote kinachoweza kutunyakua kutoka kwa mikono ya Kristo? (kif. 28) ______________________________
7. Je kuna mtu anayeweza kutunyakua kutoka katika mikono ya Baba yetu? (m.29) ________________________________________

Sasa soma **Waefeso 1:13-14** na ujibu swali la 8 hadi 9

8. Je ni kazi gani aliyoifanya Mungu ndani yetu? (kif.13) _______________
_______________________________________________
9. Je ni wakati gani ambapo tulitiwa muhuri? (kif.13) ________________
_______________________________________________

Mungu alitupa Roho mtakatifu kama hakikisho kwamba sisi ni mali yake.

***Soma "Mimi ni nani katika Kristo" katika, maelezo ya ziada #2 mwishoni mwa kitabu.***

Je unajisikiaje unaposoma hakikisho hili? Je unapata ujasiri? ________
_______________________________________________

**KUTOA SHUKURANI**

Kutokana na Yohana 10:28-29, Wewe upo katika mikono yaYesu Kristo, na wakati uo huo upo katika mikono ya Mungu Baba.

Hebu fikiri juu ya ulinzi imara ulio nao katika mikono hiyo! Si ajabu kuona kwamba inasema mara mbili kuwa hakuna anayeweza kututoa katika mikono yake.




**HEBU FIKIRI**

Dhambi ni kutenda, kusema, au kufikiri kitu ambacho ni kinyume na mapenzi ya Mungu. Ijapokuwa Mungu ananipenda, anachukia dhambi zangu.

Hebu fikiri na uandike sababu mbili zinazokufanya kuamini kwamba Mkristo ni sharti ajaribu kuepuke dhambi?

1. ______________________
______________________
______________________
2. ______________________
______________________
______________________





**WIKI HII**

Wiki hii mwombee mtu mmoja katika jamaa yenu ambaye bado hajampokea Kristo. Ombea wokovu wao. Andika majina yao hapa chini:

________________________

Je unatatizika kutafuta vifungu katika Biblia? Hapa kuna kidokezo. Kariri kwa mfululizo majina ya vitabu kumi vya kwanza katika Agano Jipya:

Mathayo
Marko
Luka
Yohana
Matendo
Warumi
1 Wakorintho
2 Wakoritho
Wagalatia
Waefeso



**KUWA IMARA**

**Soma Yohana 8-14 wiki hii**
(Sura moja kwa siku)

**Kariri Yohana 10:27-28**

*"Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata. Nami nawapa uzima wa milele; wala hawata potea kamwe wala hakuna mtu atakaye wapokonya katika mikono yangu".*

10. Soma 1Yohana 5:11-12. Je unao uzima wa milele? ________________

Tunawezaje kujua hakika kwamba tuna uzima wa milele? __________

____________________________________________________

____________________________________________________

**ONYO**

11. Sasa kwa kuwa nimeokoka, ni kwa nini nisicheze na dhambi?

Warumi 6:1-2 ________________________________________

____________________________________________________

Soma Waebrania 12:5-10 kishA ujibu swali la 12 na 13.

12. Kwa sababu nimekuwa mtoto wa Mungu, yeye hunirudi. Ni kwa nini

anafanya hivyo? (kif.6)___________________________________

____________________________________________________

13. Mungu hunirudi kwa lengo gani? (kif.10) ____________________

____________________________________________________

____________________________________________________

**MUNGU AMENIPA CHAGUO**

Siyo matakwa ya Mungu kwamba utende dhambi. Bali kama wanadamu tunakabiliwa na majaribu. Hii inamaanisha kwamba bado tuna shindana na dhambi katika maisha yetu.

Je itakuaje ikiwa utatenda dhambi? Huwezi kupoteza wokovu wako,bali unaweza kuathiri ushirika wako na Mungu. Akiwa Baba wa Upendo, ametupa njia ya kuepuka majaribu na kuweza kumkaribia iwapo tutatenda dhambi. Tutajifunza hili kwa undani katika hatua ya 3

**UCHIMBUZI WA KINA**

Soma 1 Wakoritho3:11-15. Kila Mkristo atahukumiwa kwa kazi yake, wala sio kudhibitisha kama ameokoka. Kama kazi yake itampendeza Mungu, basi atapata thawabu.

Kama sivyo, basi hatapokea thawabu maalum. (Thawabu hii si sawa na wokovu, maana wokovu alikwisha kupokea tayari. (kif. 15)

Je, utapokea thawabu au utaponea chupu chupu?

____________________________________________________

____________________________________________________




## Hatua 3
# Washindi!

Jibu KWELI (K) au SI KWELI (S)

______ Tunapojaribiwa ni hakika kwamba tutafanya dhambi kwa sababu tu dhaifu sana

______ Tukifanya dhambi na kutubu, Mungu atatusamehe.

______ Tunao maadui wa kiroho wanaotujaribu.

### TUMO VITANI

Biblia inasema kwamba Mungu hawezi kutujaribu (Yakobo 1:13). Basi hawa maadui wetu wa kiroho ni nani katika maandiko yafuatayo?

1. Yakobo 4:4 ____________________________________________

2. Wagalatia 5:17 ____________________________________________

3. 1 Petro 5:8 ____________________________________________

Tunaweza kukabiliana vipi na hawa maadui?

4. Ulimwengu (Warumi 12:2) ______________________________

5. Mwili (Wagalatia 5:16) ______________________________

6. Mwovu shetani (Yakobo 4:7) ______________________________

### TUNAWEZA KUWA WASHINDI

7. Ni nani mkuu kuliko shetani? (1 Yohana 4:4) ____________________

8. Nani aishiye ndani ya muumini? (1 Wakorintho 3:16) ______________

9. Ni nani atupaye ushindi? (1 Wakorintho 15:57) __________________

### MUNGU HUTUPA ZANA ZA KUTUWEZESHA KUWA WASHINDI

Kulingana na vifungu vifuatavyo, ni kitu gani tunachopaswa kufanya ili tuweze kuepuka majaribu?

10. Zaburi 119:11 ____________________________________________

11. Mathayo 26:41 ____________________________________________

12. Mithali 4:14-15 ____________________________________________


13. 2 Timotheo 2:22 ____________________________________________

**UCHIMBUZI WA KINA**

Tunajaribiwa sote, lakini hii haimaanishi kwamba lazima tutende dhambi.
1 Wakorintho 10:13, ina kweli tatu za kututia moyo.

1. Majaribu ni sehemu ya kuwa wanadamu, na inawezekana kuyashinda.
2. Mungu ameweka mipaka kwa majaribu. Tunaweza kuyapinga.
3. Mungu hutoa njia ya kuepuka katika kila jaribu.

Tafakari kweli hizi na kuziamini!




**KUTHIBITISHA UKWELI**

Mkristo anaweza kuyashinda majaribu. Je unaweza kukumbuka wakati fulani hivi karibuni ambapo ulikutana na jaribu na ukaweza
kulishinda kwa msaada wa Mungu?

______________________________

______________________________

______________________________

**KUREKEBISHA MAMBO**

Ninapaswa kukiri dhambi zangu mbele za Mungu. (Zaburi 32:5); lakini kuna nyakati ambazo kufanya hivyo hakutoshi. Ninalazimika kwenda hatua moja zaidi. Kama dhambi yangu imemwathiri mtu mwingine basi ni lazima nimtafute mtu huyo na kumwomba msamaha. (Yakobo 5:16; Mathayo 5:23-24)

Ninawezaje kupatana na Mungu ambaye simwoni, kabla sijapatana na jirani yangu ambaye ninamwona? (1 Yohana 5:20)

**WIKI HII**


Wiki hii mwombee rafiki yako mnayefanya kazi naye, mwanafunzi mwenzako, au jirani yako ambaye anahitaji kumpokea Kristo.

Wiki hii nitamwombea:

________________________

Kariri vitabu vingine kumi vinavyofuata katika agano jipya. Fanya marudio ya vile vitabu kumi vya mwanzo kutokana na somo lililopita:

Wafilipi
Wakolosai
1 Wathesalonike,
2 Wathesalonike
1 Timotheo,
2 Timotheo
Tito
Filemoni,
Waebrania,
Yakobo



**KUWA IMARA**

**Soma Yohana 5:21, juma hili** (soma sura moja kwa siku).

**Kariri 1 Yahana1:9**

*"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote".*

## TUNAWEZA KUSAMEHEWA

14. Kutokana na 1 Yohana 1:8, je kuna mtu ye yote, hata Mkristo, anayeweza kusema hana dhambi? ____________________________

Ushirika wa muumini na Mungu huvunjika muumini anapofanya dhambi. Hii haimfurahishi Mungu ingawaje anatupenda.Yeye hatasikiliza maombi yetu tusipokuwa tayari kukiri dhambi zetu.

15. Sasa tufanye nini ili tupate kusamehewa? (soma 1 Yohana 1:9)

______________________________________________________



**JE NAWEZAJE KUUNGAMA DHAMBI ZANGU?**

Kuungama ni zaidi ya kusema, "nilitenda dhambi." Ungamano la kweli linahitaji mambo haya:

a. Unyofu.
b. Kutubu kwa kusikitika na kutotamani kurudia dhambi tena.
c. Kumtajia Mungu dhambi niliyotenda.
d. Kuwa mwepesi wa kutambua makosa yangu. Nahitaji kutubu mara tu ninapotambua kwamba nimefanya dhambi. Nisipofanya hivyo, basi kuna hatari ya kufanya dhambi zaidi.
e. Kunyenyekea na kuomba walioathiriwa na dhambi zangu msamaha.
f. Kupokea msamaha. Hatuhitaji kuendelea kujilaumu kwa dhambi ambazo tumetubu tayari. Ni sharti tupokee msamaha wa Mungu, tukimwamini na kumshukuru. Tukatae shutuma za Shetani kwamba hatuwezi kusamehewa.

16. Kutokana na 1Yohana 1:9, ni kitu gani kinachotokea ninapokiri dhambi zangu?

a. ________________________________________________

b. ________________________________________________

**MUHTASARI**

1. Maadui wetu wa kiroho ni nani?

2. Je, tuna uwezo gani wa kuwashinda hao maadui?

3. Tufanye nini ili tupate kusamehewa iwapo tutatenda dhambi?




### Hatua ya 4
# Bwana wa vyote

Jibu KWELI (K) au SI KWELI (S)
______ Nina haki ya kuongoza maisha yangu
______ Nikimpa Kristo Maisha yangu yote, ataondoa raha zangu.
______ Najua kuyaongoza maisha yangu na hakuna mwingine aliye na haki ya kuniambia la kufanya.

**BWANA MKUBWA NI NANI?**

"BWANA" ni moja kati ya majina yanayotumika kumtambulisha Yesu. Ingawa dunia inaishi katika uasi dhidi ya Mungu siku za leo, siku moja kila goti litapigwa mbele zake na kila ulimi utakiri kwamba Yeye ni Bwana (Wafilipi 2:10-11).

1. Je, maana ya kusema: "Yesu ni Bwana katika maisha yangu" ni nini?

_______________________________________________

2. Kwa nini Kristo awe na haki ya kutawala maisha yangu?

   Wakolosai 1:16 ______________________________

   2 Wakorintho 5:15 ____________________________

   Je maisha yangu ni mali ya nani sasa? ______________________

**ITIKIO LANGU**

3. Kama mimi ni mali ya Kristo, yanipasa kumwitikia vipi, kwa mujibu wa

   2 Wakorintho 5:15 ____________________________

   _______________________________________________

4. Soma Wagalatia 2:20. Huu mstari unaweka kwa kifupi mambo muhimu katika maisha ya Mkristo. Eleza maana ya kifungu cha maneno yafuatayo:

   "Wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu". ____________

   _______________________________________________

   _______________________________________________

   "Kusulubishwa pamoja na Kristo" inamaanisha maisha yangu ya zamani yamekufa, au yamebakia nyuma yangu. Tangu sasa nina maisha mapya yenye nguvu za kushinda dhambi ndani ya Kristo.

5. Je, nawezaje kuishi katika maisha haya mapya ndani ya Kristo? Soma sehemu

   ya pili ya Wagalatia 2:20 ___________________________

   _______________________________________________

   _______________________________________________

**ANGALIA**

Kuna vitu vingi visivyo vibaya ambavyo vinaweza kuchukua nafasi ambayo Kristo ndiye anayepaswa kuchuka katika maisha yetu.

Weka alama katika vitu ambavyo vinazuia kazi ya Kristo katika maisha yako.

❏ Vitu ulivyo navyo ❏ Kazi
❏ Tama zako ❏ Marafiki
❏ Viburudisho ❏ Mazoea
❏ Tabia yako ❏ Jamii yako
❏ Mengineo ____________

____________________

**HEBU FIKIRI**

Ni maeneo gani hasa unayohitaji kusalimisha kwa Kristo?

____________________

____________________

____________________

____________________

**WIKI HII**

Malizia kukariri vitabu vifuatavyo vya agano jipya. Fanya marudio ya majina ya vitabu vile ambayo ulikwisha kukariri.

1 Petro, 2 Petro
1 Yohana, 2 Yohana, 3 Yohana
Yuda
Ufunuo

**KUISHINDA HOFU**

Je unafadhaishwa unapofikiri kuyasalimisha maisha yako yote kwa Kristo?




JE, MUNGU ANANITAKIA MEMA?

Hapa chini kuna baadhi ya vitu vinavyofanya watu wengi waogope kuyasalimisha maisha yao kwa Kristo? Weka alama kando ya vile vinavyokuathiri.

- ❏ Naogopa kwamba Yesu hajui matatizo yangu kwa hakika.
- ❏ Naogopa kwamba Kristo anaweza kuniamuru kufanya kitu ambacho siwezi kukamilisha.
- ❏ Nahofia kwamba Kristo hataniruhusu kuoa au kuolewa na mtu atakayeleta furaha katika maisha yangu.
- ❏ Nahofia kwamba Mungu ataniondolea marafiki na raha zangu.
- ❏ Ninahofia kwamba sitaweza kuwa mwaminifu, au kuyatimiliza matakwa yake.

Sasa soma 1Petro 5:6-7. Kulingana na kifungu hiki, je unafikiri kuna sababu yo yote kwako kuwa na hofu?

Ndiyo ❏ Hapana ❏



**KUWA IMARA**

**Soma Matendo 1-7**
(Sura moja kwa siku).

**Kariri Wagalatia 2:20**

*"Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu".*

6. Ni njia ipi nzuri ya kufahamu kama Kristo ni Bwana katika maisha yangu?

   Luka 6:46 ____________________________________________

7. Kwa nini ni muhimu kuyasalimisha maisha yangu kwa Kristo?

   ✓ Siwezi kuwatumikia mabwana wawili.Yanipasa kuamua kama nitamtumikia Mungu au kuutumikia Ulimwengu. Siwezi kuwapendeza wote wawili (Luka 16:13).

   ✓ Mimi ni mtumwa wa dhambi ikiwa Kristo si kiongozi wa maisha yangu (Warumi 6:16).

   ✓ Siku moja nitasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo na kutoa hesabu. (2 Wakorintho:10).

**NANI MWENYE UWEZO WA KUTAWALA MAISHA YANGU?**

| | Yesu | Mimi |
|---|---|---|
| Je ni nani anayenitakia mema katika maisha yangu? | ❏ | ❏ |
| Je ni nani anayejua yanayofaa katika maisha yangu? | ❏ | ❏ |
| Je ni nani mwenye uwezo wa kufanya mazuri maishani yangu? | ❏ | ❏ |

**NINAPASWA KUSALIMISHA NINI KWA KRISTO?**

8. Maeneo muhimu katika maisha yangu ambayo ninapaswa kuyasalimisha ni:

   Warumi 12:1____________________________________________

   Isaya 26:3____________________________________________

   Waefeso 5:15-16________________________________________


   2 Wakorintho 6-7 _______________________________________

**KUJISALIMISHA KWA KRISTO KILA SIKU**

Warumi 12:1 inatusihi tusalimishe miili yetu kwa Kristo. Maombi yafuatayo yanaweza kuwa mfano wa jinsi ya kujisalimisha kila siku.

*"Najisalimisha kwako ee Bwana.*
*Tawala ufahamu wangu na mawazo yangu*
*Tawala macho yangu na kile ninachokiona*
*Tawala masikio yangu na kile ninachokisikia.*
*Tawala ulimi wangu na kile ninachokizungumza.*
*Tawala moyo wangu, hisia zangu, na mwenendo wangu.*
*Tawala mikono yangu na kila kitu ninachokifanya.*
*Tawala miguu yangu, na kila mahali ninakokwenda.*
*Tawala mwili wangu, kwa maana ni hekalu lako.*
*Naomba unijaze kwa Roho wako Mtakatifu.*
*Ninataka kukutii wewe.*
*Ninataka kuyatenda mapenzi yako."*





# Hatua ya 5
# Kuishi katika Roho

Jibu KWELI (K) au SI KWELI (S)
______ Roho Mtakatifu ni "nguvu" ya Mungu?
______ Roho Mtakatifu anatupa ufahamu wa kuelewa dhambi zetu.
______ Roho Mtakatifu anaishi ndani ya watoto wa Mungu.

**KAZI YA KWANZA YA ROHO MTAKATIFU**

Yesu Kristo alimtuma Roho Mtakatifu (Roho wa kweli) alipo paa juu mbinguni kwa Baba ili apate kumshuhudia Yeye. (Yohana 15:26)

1. Kutokana na Yohana 16:8-9, Roho Mtakatifu ana kazi gani kwa wasioamini? ______________________________

2. Roho Mtakatifu ndiye amfanyaye mtu aliyempokea Yesu kuzaliwa mara ya pili. (Yohana 3:3-8). Je kuzaliwa mara ya pili inamaana gani kwako?

   ______________________________

   ______________________________

   Kwa kuongezea, Roho Mtakatifu anafanya mambo mengine kwa mtu ambaye amempokea Kristo, kama tutakavyo ona hapo chini.

3. Kutokana na 1Wakorintho 12:12-13, sote ______________ katika mwili mmoja kwa Roho.

   Ubatizo wa Roho haina maana sawa na ubatizo wa maji, bali ni Roho Mtakatifu kutufanya washirika wa mwili wa Kristo, ambalo ni kanisa linaloundwa na waumini wa kweli Ulimwenguni kote.

4. Kutokana na Waefeso 1:13, ____________ kwa Roho yule wa ahadi

   Kuwekwa 'muhuri' kwa Roho inamaanisha kwamba mtoto wa Mungu aliyezaliwa ni mali ya Mungu (m. 14).

5. Kutokana na 1 Wakorintho 3:16, Mkristo ni hekalu la Mungu, na Roho Mtakatifu ______________________ ndani yake. Hii ina maana kwamba Roho Mtakatifu anakaa ndani ya Mkristo wakati wote.



**MUHTASARI KWA KAZI YA MWANZO ZA ROHO MTAKATIFU**

- ✓ Anashuhudia juu ya dhambi
- ✓ Anasababisha kuzaliwa kwa mara ya pili
- ✓ Ana tubatiza kuwa mwili wa Kristo
- ✓ Anatutia muhuri wa milele
- ✓ Anakaa mwilini mwetu

**UCHIMBUZI WA KINA**

Kutokana na 1 Wkorintho 6:11' je Roho Mtakatifu ni nani?

______________________

______________________

______________________

Angalia pia Matendo 5:3-4

**HEBU FIKIRI**

Waefeso 1:14 inasema kwamba Roho Mtakatifu mwenyewe ndiye arabuni ya ukombozi wetu.

Je ukweli huu unakufanya kuhisi vipi?

______________________

______________________

______________________

**ITIKIO LANGU**

Kwa kujua kwamba miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu wa Mungu, je tunapaswa kuitunza miili yetu namna gani?

Angalia 1 Wakorintho 6:19-20

______________________

______________________

______________________

______________________

## KAZI YA KUENDELEA YA ROHO MTAKATIFU

6. Je Kristo aliahidi nini kuhusu ufahamu wa kiroho, kulingana na

   Yohana 14:26? ________________________________________________

   ________________________________________________

   Ni furaha kubwa sana kwa kujua kwamba Roho wa Kristo mwenyewe hutufundisha!

7. Roho Mtakatifu anatufahamu binafsi. Je ni kitu gani kingine

   anachomtendea muumini, kutokana na Warumi 8:26-27______________

   ________________________________________________

8. Warumi 8:14, inasema kwamba Roho Mtakatifu humwongoza Mkristo. Ili kuongozwa na Roho Mtakatifu, Mkristo anastahili:

   Waefeso 5:18________________________________________________

   Wagalatia 5:16______________________________________________

   Kujazwa na Roho Mtakatifu au kutembea katika Roho ina maana kwamba Mkristo ametawaliwa na kuongozwa na Roho Mtakatifu. Hii inadhihirishwa na tunda lililotajwa katika Wagalatia 5:22-23




### NAWEZAJE KUJAZWA NA ROHO MTAKATIFU?

- Unapotambua kwamba umetenda dhambi, unawajibika kukiri mbele za Mungu.Usisubiri dhambi ziongezeka (1 Yohana 1:9). Ni jambo la busara kukubali kwa imani msamaha ambao Mungu anakupa.
- Jipeane mwenyewe kwa Mungu. Mruhusu atawale maisha yako, ukijinyenyekeza kwa mapenzi yake. (Warumi 6:13). Fanya marudio ya maombi katika somo lililopita.
- Kwa imani hisi uwepo wa Roho Mtakatifu, yaani uamini kwamba ndiye anayekutawala. Anza kutenda kwa imani.

## MUHTASARI WA KAZI YA ROHO MTAKATIFU KWA MUUMINI

Anamfundisha muumini
Anamwombea muumini
Anamwongoza muumini
Anamjaza muumini
Anamtukuza Kristo (Yohana 16:13-14)


**WIKI HII**



Mshuhudie mtu mmoja jinsi ulivyo weza kumjua Kristo. Hii ingekua vizuri kwa mtu ambaye umekuwa ukimwombea.

**UCHIMBUZI WA KINA**

Soma Yuda 20. Ina maanisha nini kuomba kwa Roho mtakatifu? Angalia swali la 8



**KUWA IMARA**

**Soma Matendo 8-14**
(sura moja kwa siku)

**Kariri 1 Wakorintho 12:13**

*"Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani,ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja".*



## Hatua ya 6
# Mungu Hunena Nami

Jibu KWELI (K) au SI KWELI(S)
______ Karibu Biblia yote ina chanzo chake kutoka kwa Mungu
______ Yeyote aulizaye msaada wa Mungu anaweza kuelewa Biblia.
______ Ni muhimu kutafakari Biblia ili kupata manufaa makubwa kutokana nayo.

### BIBLIA NI NINI?

1. Je 2 Timotheo 3:16 inasemaje kuhusu chanzo cha Biblia? ______________
________________________________________________________________

Neno "limevuviwa" linapatikana katika tafsiri zingine likiwa na maana ya "kupuliziwa pumzi ya uhai na Mungu." Hii inatuambia nini kuhusu Neno la Mungu? ________________________________________________

Huu mstari unasema kwamba__________________andiko lina pumzi ya Mungu. Kama hivi ndivyo ilivyo, je kunaweza kuwa na kosa ndani yake?
________________________________________________________________

2. Je, Biblia inatofautiana na vitabu vingine kwa namna gani?
Waebrania 4:12 ________________________________________________

3. Eleza jinsi Biblia inavyotumika kama upanga katika maisha yako.
Waebrania 4:12) ______________________________________________
________________________________________________________________

### KUSUDI LA BIBLIA

4. Biblia inakulisha kiroho. Je Biblia inafananishwa na nini katika
1 Petro2:2? ________________________________________________

Je ni kitu gani kinachoweza kutokea kwa Mkristo anayepuuza kusoma Biblia? ________________________________________________

5. Biblia inakuongoza katika maisha yako ya kila siku. Je, Biblia inafananishwa na nini katika Zaburi 119: 105? ______________________

Je taa ina matumizi gani? ________________________________________

***Tunaishi katika nyakati za udanganyifu. Kuna "waalimu" wengi, makanisa mengi na marafiki wengi wanaotaka kutupa mashauri. Tutajuaje anayezungumza ukweli? Mungu ametupa Biblia kwa kusudi la kuangaza ufahamu wetu na kutusaidia kuchambua mashauri tunayopewa.***

6. Biblia inakusaidia usitende dhambi. (Zaburi 119:9). Je maana ya "Moyoni mwangu nimeliweka Neno lako" ni nini? ____________________________
________________________________________________________________

**WIKI HII**

Unaendeleaje Katika kusoma Biblia kwa mujibu wa kazi uliyopewa kufanya katika kila somo? Je, unasoma Sura moja kila siku?

Ndiyo ❏ La ❏

Je, unaposoma Biblia umetambua kwamba nguvu zake zimegusa moyo wako au kubadili maisha yako?

Ndiyo ❏ La ❏

Hebu mwambie mtu mwingine yale unayojifunza kutokana na yale unayosoma. Kama hujaanza kusoma Biblia yako mara kwa mara, basi mbona usianze leo?

Najitolea kusoma Biblia yangu kwa uwezo wake Mungu (pendekezo ni kusoma sura moja kwa siku)

Tarehe ____________________



Hebu kariri kwa mfululizo majina ya vitabu 14 vya kwanza katika Agano La Kale:

Mwanzo
Kutoka
Mambo ya Walawi
Hesabu
Kumbukumbu La Torati
Yoshua
Waamuzi
Ruthu
1 Samweli na 2 Samweli
1 na 2 Wafalme
1 na 2 Mambo ya Nyakati

**TAFAKARI MAANDIKO**

Yoshua 1:8 inatuamuru kutafakari maandiko mchana na usiku, yaani wakati wote. Tunapendekeza njia zifuatazo katika kutafakari maandiko ya Biblia.




Nakili kifungu cha maandiko katika karatasi ndogo ya 3x5 (au kwenye kitabu cha kumbukumbu) kutoka kwenye usomaji wako wa Biblia kila siku.

Kibebe karatasi hicho kwenye kifuko, au weka pahali pa wazi, kama vile kwa kioo au juu ya chombo cha kufanyia vitu baridi *(refrigerator)* ili upate kufanya marudio kwa vifungu hivyo kila wakati.

Unapotafakari maandiko jaribu kujiuliza hivi:


- Mungu anataka kunifundisha nini?
- Nitawezaje kulitendea kazi neno hili kila siku katika maisha yangu?

**HEBU FIKIRI**

Je Biblia ina mamlaka ya kipekee katika maisha yako? Soma Matendo 17:10-11. Je waumini wa Beroya walikuwa na tabia gani nzuri inayoweza kuigwa?

______________________

______________________



**KUWA IMARA**

**Soma Matendo 14-21**
(sura moja kwa siku).

**Kariri 2 Timotheo3:16 –17**

*"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema."*

7. Biblia inakusaidia kukua katika maisha ya Kikristo. Kutokana na 2 Timotheo 3:16-17. Biblia inafaa kwa:

______________________ ______________________

______________________ ______________________

Mtu ambaye anaruhusu Biblia kumwongoza "ataimarika katika kila kazi njema." Uwe mwangalifu sana na watu wanaosema Biblia pekee haitoshi, na wakikutia moyo kutafuta ndoto na, na mafunuo kama nyongeza. Biblia inatosha!

8. Je, kuna wakati mwingine ambapo unaona kuwa ni vigumu kuwa na imani? Soma Warumi 10:17 kisha uyajibu maswali yafuatayo:

Je, tunapataje imani? ______________________

Je, tunawezaje kuongeza imani yetu? ______________________

**YALIYOMO KATIKA BIBLIA** Biblia imegawanywa kwa sehemu mbili:

| **AGANO LA KALE**<br>Vitabu 39 | **AGANO JIPYA**<br>Vitabu 27 |
|---|---|
| Sheria (Mwanzo hadi Kumbukumbu la Torati) | Maisha ya Kristo ( Injili 4) |
| Historia ya Israeli (Yoshua hadi Esta) | Kukua kwa Kanisa.(Matendo) |
| Mashairi (Ayubu hadi Wimbo Ulio Bora) | Mafundisho (Nyaraka) |
| Manabii (Isaya hadi Malaki) | Unabii( Ufunuo) |

**JINSI YA KUFAIDIKA KUTOKANA NA BIBLIA**

**Sikiliza:** Shiriki katika Kanisa ambalo neno la Mungu linafundishwa kwa uaminifu. (Ufunuo 1:3; Waebrania 10:24-25)

**Soma:** Je unasoma Biblia yako kila siku? Andika katika daftari kile unachojifunza kila siku katika maisha yako. (Tazama Mambo ya ziada # 4). Ni vizuri kuanza kwa kusoma kitabu cha Yohana, Matendo, 1 Yohana, na Warumi.

**Tafakari:** Angalia kuhusu "KUTAFAKARI MAANDIKO" ilivyoelezwa hapa kando. Kumbuka kwamba dini nyingi na vikundi vingi vina jinsi nyingi za kutafakari. Wanajaribu kuondoa mawazo yote katika akili zao na kurudiarudia maneno fulani mara nyingi hadi wakawa kama wamepagawa. Hao huona kana kwamba wamo safarini kwa kusudi la kupata mwongozo wa kiroho. Hi sivyo ilivyo katika kutafakari Biblia, bali ni kupiga ramli, uchawi, na kuabudu sanamu. Hii inamchukiza Mungu sana (Kumbukumbu 18:9-13). Kutafakari kibiblia kunahusu kuwazia na kunena maneno ya Mungu.

**Kariri:** Kuna mstari wa kukariri katika kila somo. Ni muhimu sana kumaliza kazi hii kwa sababu kama una mstari ambayo umekariri, basi itakuwa rahisi kuukumbuka badaye na kuutumia.

**Tii:** Andika kwa maneno yako mwenyewe wazo kuu katika Yakobo 1:22

______________________

Ezra alifanya nini na maandiko? (Ezra 7:10). Andika mambo matatu.

1. ______________________
2. ______________________
3. ______________________



## Hatua ya 7
# Kuzungumza na Mungu

Jibu KWELI (K) au SI KWELI(S)

______ Karibu Biblia yote ina chanzo chake kutoka kwa Mungu

______ Yeyote aulizaye msaada wa Mungu anaweza kuelewa Biblia.

______ Ni muhimu kutafakari Biblia ili kupata manufaa makubwa kutokana nayo.

**MAOMBI NI NINI?**

Maombi ni kuwasiliana na Mungu. Ni rahisi kama vile kuzungumza na rafiki. Unaweza kuzungumza na Mungu kwa ujasiri kuhusu jambo lo lote, liwe hofu au hitaji. Maombi ni mawasiliano ya karibu sana na Mungu.

1. Je Mungu ametupatia nini katika Yeremia 33:3? ________________

   ________________________________________

   Maombi ni njia ya kueleza wazi wazi mambo yaliyomo moyoni mwako kwa rafiki yako anayekusikiliza kwa makini. Je, Mungu ameahidi

   kuitikia maombi yako vipi? ________________________

   ________________________________________

   Je kuna nyakati ambapo Mungu huwa na shughuli na hwa hivyo hawezi kujibu maombi? Ndiyo ❏ La ❏

2. Maombi ni njia mojawapo ya kujilinda. Je Yesu alitoa ushauri gani kwa wanafunzi wake ili wasije wakaingia majaribuni?

   Mathayo26:41 ________________________________

3. Ni hatari zipi tunazohitaji kuepuka tunapoomba?

   Mathayo 6:5 ________________________________

   Mathayo 6:7 ________________________________

   Je tafsiri yako kuhusu maneno “marudio yasiyo na maana” (yaani

   kupayukapayuka kama wapagani) ni nini? ________________

   ________________________________________

**TUOMBE VIPI?**

4. Zaburi inatupa sababu nyingi za kumsifu Mungu. Kwa mfano,

   Zaburi 106:1 inakupa sababu zipi za kumsifu Mungu? __________

   ________________________________________

5. Katika Wafilipi 4:6 unapaswa kufanya nini badala ya kuwa na hofu?

   ________________________________________

**FIKIRI TENA**

Tunapaswa kuelekeza nia gani kwa Mungu? Waebrania 4:16?

________________

________________

Kwa mawazo yako, ni kwa nini tuwe na ujasiri kwa Mungu?

________________

________________

*“Yatupasa tuombe tunapokuwa na hamu ya kuomba maana ni dhambi kupoteza wakati wa thamani kama huo.Yatupasa kuomba wakati hatuna hamu ya kuomba, maana inaweza kuwa hatari sana kukaa katika hali hiyo.”*

*Charles H. Spurgeon*

**WIKI HII**

Kariri mfululizo wa vitabu vifuatavyo vya Agano la kale, na kufanya marudio kwa yale uliyojifunza mbeleni.



Ezra
Nehemia
Esta
Ayubu
Zaburi
Mithali
Muhubiri
Wimbo Ulio Bora
Isaya
Yeremia
Maombolezo
Ezekieli
Danieli

**WIKI HII**

1 Timotheo 2:1 inatuagiza kwamba "dua na sala, na maombezi na shukrani zifanyike kwa ajili ya watu wote."

Je una orodha ya maombi yako inayokukumbusha mtu unayestahili kumwombea?

Orodhesha maombi yako katika karatasi au daftari.

Orodha yako inaweza kuhusisha:

- Watu wa jamaa yako
- Rafiki wako
- Kaka na dada katika imani
- Watumishi wa Mungu (mchungaji wako, na watumishi wengine)
- Viongozi wa nchi yako na jamii kwa ujumla.
- Watu ambao wamekudhuru
- Watu ambao ungependa wampokee Kristo
- Malengo na maendeleo yako binafsi

6. Kutokana na Wafilipi 4:6, tunapaswa kuwa na nia gani tunapoomba jambo lo lote kutoka kwa Mungu? ____________________

   Tunaonyesha imani yetu kwa Mungu kwa jibu ambalo atatupa kwa ombi letu tunapoomba na "kushukuru". Ndiyo maana mstari wa 7 unasema tutapata ____________ katika mioyo yetu, tunapoweka mizigo yetu katika mikono ya yule mwenye uwezo wa kutusaidia kwa shida zetu.

7. Je kuomba bila kukoma kuna maanisha nini? (1 Watesalonike5: 17)

   ____________________

   Je, kuomba wakati wote inamaanisha kwamba unaweza kuomba mahali popote, kama vile kazini, unaposafiri, na kadhalika? ____________

   ____________________



**Maombi yetu yahusishe mambo haya:**

Kumwabudu Mungu na kumsifu kwa jinsi alivyo.

Kukiri dhambi zako ili zisiweze kuzuia ushirika wako na Mungu.

Maombi kwa ajili ya mahitaji yako na maombezi kwa ajili ya watu wengine.

Shukurani. Je, Mungu amekufanyia nini? Usiwe mtu asiye na shukurani. Tuwe watu wenye shukurani.

8. Kulingana na Yohana 14:13 ni lazima tuombe kwa jina la ____________

9. Tunaweza kujifunza nini kuhusu maombi kutokana na vifungu vifuatavyo?

   Zaburi 66:18 ____________________

   1 Yohana 5:14-15 ____________________

   Matayo 21:22 ____________________

10. Waefeso 3:20 inakupa moyo vipi katika imani yako? ____________

    ____________________


    ____________________

**MUNGU HUJIBU MAOMBI YAKO**

Tumeona kwamba Mungu ameahidi kujibu maombi yako. Lakini atajibu vipi? Mtu mmoja alisema kwamba Mungu anajibu kwa jinsi tatu:

- Wakati mwingine husema "Ndiyo".
- Wakati mwingine husema "hapana" kwa faida yetu sisi.
- Wakati mwingine husema "Subiri kidogo".

**KUWA IMARA**



**Soma**
**Matendo 22-28**
(sura moja kwa siku)

**Kariri Wafilipi 4:6-7**

*"Msijisumbue kwa jambo lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru., haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu."*




## Hatua ya 8

# Kukutana na Mungu Kila Siku

Jibu KWELI (K) au SI KWELI (S)

______ Ni muhimu kusoma Biblia na kuomba kila siku.
______ Mtu anatakiwa kusoma vifungu vingi vya Biblia kwa siku.
______ Mungu anataka kutubadilisha siku kwa siku kwa neno lake

**MUDA WA IBADA NI NINI?**

Muda wa ibada  ni ahadi tuliyokubaliana na Mungu wetu kwa kila siku. Muda huu unastahili kwa wa kila siku, maana kujenga ushirika wetu na Mungu huchukua muda.  Ukomavu hauji kwa mara moja tu, bali hupaliliwa siku baada ya siku, hatua moja kila wakati.

> ***"Bwana asubuhi utaisikia sauti yangu, Asubuhi nitakupangia dua yangu na kutazamia." Zaburi 5:3***

Watu wengine wanauita "wakati wa utulivu" maana ni wakati wa kumsubiri Mungu ili azungumze nasi kwa neno lake, nasi tuweze kujibu kwa maombi.

**NI MUHIMU**

Mbona ni muhimu kutenga muda wa ibada kila siku?

Yoshua 1:8 ______________________________

Zaburi 63:1 ______________________________

Mathayo 4:4 ______________________________

Je, kuwa na muda na Mungu kila siku ni muhimu au ni wazo zuri tu (yaani ukiwa na muda)? ______________________________

______________________________

**NI WAKATI GANI NA SEHEMU GANI UTAKAYOFANYIA IBADA YAKO?**

Mara nyingi wakati mzuri ni asubuhi. Hii inatusaidia kuanza siku yetu na Mungu. Watu kama Daudi na Kristo walitenga muda maalum wakati wa asubuhi (Zaburi 5:3 na Marko 1:35).  Hii itatulazimu kuamka mapema kuliko kawaida, lakini tutaona matokeo yake. Wengine wanapenda muda wa jioni (Zaburi 63:6) au wakati mwingine mchana wanapojua kwamba wanaweza kutimiza "agano" na Mungu.

Kwa wakati wowote utakaochagua, tafuta mahali patulivu, ambapo unaweza kutumia muda wako bila kusumbuliwa. Ili kufanikiwa vyema ni vizuri kuamka kabla ya watu wengine, kufunga mlango wa chumba chako, au kwenda nje.

Weka muda wa ibada sasa.

*Saa* ____________ *Nitaamka saa* ____________

*Mahali* ______________________________

**HEBU FIKIRI**

Waebrania 4:12 inailinganisha Biblia na "upanga ukatao kuwili"

Wakati mwingine kusoma haifariji, kwa sababu hupenya maishani mwetu na kutuonyesha jinsi tulivyo ili tuone haja ya kujirekebisha.

Je umewahi kumshukuru Mungu kwa uwezo wa neno lake kufanya hivyo?

**JUMA HILI**

Kariri majina ya vitabu vifuatavyo, vya Agano la kale ukifanya marudi kwa yale  uliyokariri hapo  mbeleni.

Hosea
Yoeli
Amosi
Obadia
Yona
Mika
Nahumu
Habakuki
Zefania
Hagai
Zakaria
Malaki



**TARATIBU KATIKA KUSOMA BIBLIA**

Tunapendekeza uanze kusoma Biblia katika Agano Jipya. Soma kutoka katika kitabu kimoja kila siku mpaka ukimalize.


Unaweza kuanza kusoma vitabu vya Biblia kwa kutumia utaratibu ufuatao:

Yohana
Matendo
1 Yohana
Warumi
Yakobo
Wafilipi

Mambo ya ziada #5 inakupa orodha ya masomo kwa mwaka mzima.

Baada ya kumaliza kusoma kitabu kimoja, jaribu kusoma Zaburi na Mithali kabla kuanza kusoma kitabu kingine.

**KUWA IMARA**



**Soma**
**1Yohana 1-5,**
**Zaburi 1 na 5**
(sura moja kwa siku)

**Kariri Yoshua 1:8**

*"Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawa sawa na maneno yote yaliyoandikwa humo; maana ndipo utakapoifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapositawi sana"*

Mambo ya ziada #4 immeleza kwa mhtasari jinsi ya kufanya ibada.

Kata ukurasa huo na kuuweka katika Biblia yako. Itakuwa na manufaa kwako unapokuwa na agano na Mungu kila siku.

## MAMBO YA KUHUSISHA KATIKA IBADA YAKO

### *Andaa moyo wako:*

Unastahili kwenda mbele za Mungu ukiwa na nia gani?

Zaburi 139:23-24 ______________________________

Zaburi 119:18 ______________________________

Zaburi 5:3 ______________________________

Waebrania 4:16 ______________________________

### *Jifunze Neno la Mungu*

Katika Yohana 5:39, tunaona kwamba viongozi wa Kiyahudi walihitajika kuyajua maandiko.Waberoya katika Matendo 17:11, waliyachunguza maandiko walipoyapokea, na mwimbaji wa Zaburi akasema, nimeyachunguza mausia yako…Nitazitafakari shuhuda zako.(Zaburi119:94, 95). Hii inaonyesha kwamba usome tu, bali uyachunguze ili ujifunze maana na kusudi la Mungu kunena nawe.

Kwanza, jifunze somo fupi (si zaidi ya sura).Wakati mwingine ni vyema kusoma aya fupi mara kwa mara, kuliko kusoma sura nzima. Kwa njia hiyo unaweza kuchanganua vizuri.



**Jinsi Ya Kujifunza Biblia**

Somo: ______________________

✓ Ni kitu gani kimekuvutia sana kutokana na somo hili?

✓ Wazo gani lililo kuu katika somo hili?

✓ Wazo hili lina maana gani katika maisha yako?

✓ Maswali yafuatayo yanaweza kukusaidia kupata mambo mengi katika aya.

- Je kuna amri ye yote ya kutii?
- Je kuna mfano wowote wa kuigwa?
- Je kuna dhambi yo yote ya kuepuka?
- Je kuna ahadi yo yote ya kuweka?

✎ Tafuta daftari ya kutumia kwa wakati wako wa ibada. Tumia taratibu uliyopewa hapo juu kwa kusoma Biblia yako.

**MAPENDEKEZO YA JINSI YA KUFANYA KWA VITENDO**

1. Tenga muda wako wa Ibada. Usiwe na haraka.
2. Weka kipaumbele katika muda wako na Mungu. Usikose, kama unaruka siku, usikate tamaa, lakini usikose kwa siku ya pili.
3. Jaribu kusoma sura moja kwa siku. Kwa wakati soma kidogo ili upate kujifunza vizuri. Na wakati mwingine utahitaji kusoma zaidi.
4. Weka alama katika Biblia yako, pigia mstari mistari ya muhimu ili uweze kuipata baadaye.
5. Jaribu kuandika kwa maneno yako mwenyewe ile mistari ya muhimu, ili uweze kuelewa vizuri.
6. Ni vigumu kusoma au kuomba kwa nguvu, au kuomba wakati mtu amesimama. Sio vizuri kuomba wakati umelala kitandani. Unaweza kushikwa na usingizi. Mwombe Mungu apate kukusaidia .
7. Pata kitabu cha kuandika matokeo ya masomo yako na maombi yako

## Omba

Omba kwa kulingana na kifungu cha Biblia ulichosoma. Itikia Mungu kwa kumwambia kile unachotaka kufanya kulingana na kifungu hicho, ukihusisha mambo haya:

- Kuungama, unapogundua uchafu wote katika maisha yako.
- Mwabudu Mungu kwa jinsi alivyo (Zaburi inaweza kukusaidia kukuza sifa).
- Umtukuze Mungu kwa kile anachokifanya.
- Mshukuru Mungu kwa yote afanyayo.
- Ombea mahitaji yako.

## Mwimbie Bwana

Nyimbo huinua roho yako na kukutia hamu ya kumwabudu Mungu. Imba pambio na tenzi mara kwa mara, au hata kwa siku nzima, wala sio tu kwa ibada. Waefeso 5:19. Ukipenda basi endeleza ubinja wa pambio.

## Fanya kwa vitendo

Yakobo 1:22, inatutahadharisha tuwe "watendaji wa neno wala si wasikiaji tu." Kusoma Biblia bila kutenda ni sawa na mtu anayeangalia uso wake katika kioo na kuondoka bila kuondoa uchafu ambayo ameona kwa uso wake. Haina maana yo yote kusoma Biblia bila kuwa tayari kujisalimisha kwa kutenda inavyosema.

Hii haimaanishi kwamba tuache kusoma Biblia tunapohisi kwamba tumeasi. Tunastahili kusoma Biblia hata zaidi wakati kama huo tukimwomba Mungu abadilishe mioyo yetu. Usikubalie maadui wa kiroho wakuzuie kusoma Biblia.(Angalia hatua ya 5)

## Tafakari na Kukariri

Nakili mstari kutoka kwenye kifungu ulichokisoma ili upate kuutafakari kila wakati. Jaribu kukariri. Kwa njia hii Mungu atakusaidia kukataa dhambi.

---

**MARUDIO: RATIBA RAHISI KWA MUDA WAKO WA IBADA**

1. **Andaa moyo wako**
   - Jichunguze
   - Ungama dhambi zako
   - Omba Mungu akupe ufahamu




2. **Chunguza Biblia**
   - Ni kitu gani kimekuvutia sana?
   - Je wazo kuu ni lipi?
   - Je lina maana gani kwako?
3. **Omba Bwana**
   - Zungumza na Mungu kuhusiana na yale uliyosoma
   - Mwabudu Mungu kwa jinsi alivyo
   - Mshukuru Mungu kwa yale aliyoyatenda
   - Mwombe Mungu ukitumia orodha uliyotayarisha
4. **Mwimbie Bwana**

   Imba wimbo au tenzi. Hii itainua moyo wako na kukusaidi kumsifu Mungu.
5. **Weka katika vitendo**

   Utafanya nini leo ili kuweka uliyojifunza katika vitendo katika maisha yako?
6. **Tafakari na Kukariri**

   Chagua kifungu kutoka kwa aya uliyosoma ili uweze kukitafakari, na kukikariri. Andika kifungu hicho katika daftari au karatasi ili uweze kutembea nayo wakati wa mchana.



## Hatua ya 9
# Kanisa Langu

Jibu KWELI (K) au SI KWELI(S)

_____ Kanisa ni jengo tu.

_____ Kanisa ni jamii ya waumini.

_____ Mimi sihitaji kanisa kwa sababu ninasoma Biblia na kusikiliza vipindi vya Kikristo katika Radio na Runinga.

**KANISA NI NINI?**

Bwana Yesu alisema katika Mathayo 16:18: "… Nitalijenga kanisa langu…" Kristo aliongea kwa wakati ujao (nitalijenga) na kulizungumzia kanisa kama mali yake (kanisa langu). Kanisa hili ambalo Kristo angejenga tayari lipo na linaendelea kukua. Nu uwepo wa Kristo unaoonekana ulimwenguni leo.

Kwa maana nyingine, kanisa lipo ulimwenguni pote, na pia lipo mahali pamoja (Mathayo16:18, Matendo 13:1).

**KANISA LA JUMLA**

Kanisa la jumla ni mwili lisilo la kawaida ambalo linaongozwa na Kristo. Limeundwa na wale wote ambao wamezaliwa mara ya pili tangu siku ile ya Pentekote hadi siku ambapo kanisa litanyakuliwa.

1. Je kanisa linafananishwa na kitu gani? (1 Wakorintho12:27) ________

 ______________________________________________________________

2. Ni nani walio katika mwili huu (kanisa)? Kanisa linaundwa na waumini wote katika Yesu Kristo ambao wamefanywa upya na Roho Mtakatifu wa Mungu (1 Wakorintho 12:13).

3. Je Mungu ametoa nini kwa viungo vya kanisa? Warumi 12:4-8

 ______________________________________________________________

4. Nani kichwa cha kanisa? Waefeso 4:15 __________________________

5. Kutokana na Waefeso1:12, ni kwa nini kanisa lipo? _______________

 ______________________________________________________________

6. Je kanisa lina kazi gani? Mathayo 28:18-20 ______________________

 ______________________________________________________________

**KANISA LA MAHALI**

Kanisa la mahali ni kikundi cha watu waliozaliwa mara ya pili, wakabatizwa, na wana ushirika wa pamoja kwa ajili ya kumtukuza Mungu, kutiana moyo, na kutangaza habari njema.

**WIKI HII**

Kwa kuimarisha ushirika wako na ndugu katika kanisa, anza wiki hii kwa kumkaribisha mmoja wao nyumbani kwako au kwa chakula.



**HEBU FIKIRI**

Mungu amempa kila muumini karama za kiroho. Warumi 12; Waefeso 4:11 na 1 Wakorintho 12 zinazungumzia karama. Kwa mfano baadhi ya karama zilizozungumziwa ni:

- Huduma
- Kufundisha
- Kutoa
- Kushauri
- Kuhubiri
- Kuchunga
- Imani
- Hekima
- Kurehemu
- Kuongoza

Je unajua karama yako ni ipi? Kama jibu ni hapana, unaweza kujua kwa kuomba, kuhudumu katika kanisa, na kuuliza wenzako wapate kukuambia kipawa chako.

**HEBU FIKIRI**

Orodhesha visababu ambavyo waamini wengine hutumia kwa kutofika kanisani (mkusanyiko).

________________________

________________________

________________________

________________________

________________________

Sababu ya kutokuhudhuria kwao haswa ni lipi? Waebrania 10:25

________________________

________________________


________________________

________________________

________________________

**WIKI HII**

Orodhesha majina ya viongozi wa kanisa lako, na kuombea moja wao kila siku katika juma hili.



**KUWA IMARA**

**Soma Warumi 1-4 (soma kila sura kwa siku mbili ili uweze kulelewa vizuri)**

**Kariri Waebrania 10:24-25**

***"Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kua inakaribia."***

7. Soma Waebrania 10:24-25. Je Biblia inafundisha kwamba muumini anastahili kuwa na kanisa analoshiriki?

   Ndiyo ❑ Hapana ❑ Kwa sababu gani? ____________________

   ________________________________________________

   Tunawezaje kuhimizana katika upendo na kazi nzuri? ____________

   ________________________________________________

8. Waumini wa kanisa la Yerusalemu walifanya nini pamoja katika kanisa?

   Matendo 2:42 ________________________________________

   ________________________________________________

9. Kama wewe ni sehemu ya kanisa, basi unawajibika kulisaidia. Utasaidia kanisa lako kwa njia gania?

   Wagalatia 6:12 ______________________________________

   Wagalatia 6:10 ______________________________________

   1 Petro 4:10 ________________________________________

   2 Wakorintho 9:7 ____________________________________

> Katika 1Timotheo 3:1-7 na Tito1:5-9, Biblia imeweka matakwa kwa viongozi wa kanisa. Soma hivi vifungu. Inawezekana huna mpango wa kuwa kiongozi, lakini kila mkristo anatakiwa kutamani kuwa na hizi tabia zilizotajwa katika vifungu hivi.

10. Kwa sababu viongozi wamewekwa kanisani na Mungu, tuwe na nia

    gani juu yao? 1 Wathesalonike 5:12-13 ____________________

    ________________________________________________

    Waebrania 13:17 ______________________________________

11. Eleza moja kati ya wajibu wa kanisa kwa washirika, kutokana na

    Wagalatia 6:1-2 ______________________________________

    ________________________________________________

12. Unastahili kuwa na nia gani kwa kumrekebisha ndugu anayekosa

    mwelekeo? Fungu la 1,2 ________________________________

    ________________________________________________

Kwa sababu kanisa ni kama jamaa, lina wajibu kwa ukuaji wa watu wake. Nidhamu huhitajika mara nyingine ili kudumisha ushuhuda na kutunza usafi wa kanisa. Hili ni tendo la pendo na nia njema kwa washiriki wa kanisa. Mungu hutumia nidhamu kama mojawapo ya vitu vya "kuhimizana katika upendo na kazi nzuri".



## Hatua ya 10
# Kushuhudia

Jibu KWELI (K) au SI KWELI (S)
____Ni muhimu kuwaambia wengine habari njema, maana wengi wanaelekea kuzimu.
____Naweza kuwahubiria jamaa yangu na rafiki zangu na kupata matokeo mazuri.
____Lazima nisubiri nipate mafunzo ya jinsi ya kushuhudia ndipo

Moja kati ya wajibu wa mwamini ni kushuhudia wengine juu ya imani yake katika Kristo. Kushuhudia au kuhubiri injili ni kuwaambia wengine mpango wa wokovu ili wapate kumpokea Kristo.

**HAJA YA KUSHUHUDIA**

Mwanadamu ametegwa na dhambi, kama tulivyoona katika somo la kwanza. "Hakuna aliye mwema hata mmoja…wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" (Warumi 3:10, 23).

1. Mathayo 7:13-14 inazungumzia milango miwili inayowakilisha hatima mbili tofauti katika maisha. Kulingana na mistari hii, je ni makao gani yatakayokuwa na watu wengi?

 ____________________________________________

2. Je Yohana 3:18 inasemaje juu ya wale ambao hawamwamini Kristo?

 ____________________________________________

3. Kinyume chake ni kwamba mwamini ni ________________________
 2 Wakorintho5:17)

**TUMEPEWA KAZI MAALUM**

4. Mungu ametuteua kuwa mabalozi wake. Ni kazi gani aliyotupa kama mabalozi wake, kutokana na 2 Wakorintho5:20? __________________

 ____________________________________________

5. Soma Mathayo 5:14-16. Pamoja na kuwa mabalozi, Kristo anatuita

 ______________________________ (kifungu cha 14).

6. Kusema sisi ni "mwanga wa ulimwengu" kuna maana gani kwako ?

 ____________________________________________

 ____________________________________________

7. Kwa kinyume, kuweka taa chini ya bakuli ni nini? (kifufngu cha 15)

 ____________________________________________

 ____________________________________________

**HEBU WAZIA**

Je, waona haya kuwaambia wengine habari njema ya Kristo? Kama ni hivyo, basi soma Warumi 1:16

Kwa nini Paulo hakuionea haya injili?

________________________

________________________

________________________



**WIKI HII**

Unahisi kuwajibika kumweleza nani habari njema? Andika majina yao hapa chini.

Jamaa yako:

________________________

________________________

________________________

________________________

Marafiki na wengine unaowafahamu

________________________

________________________

________________________

________________________

Waombee mara kwa mara na kuzungumza nao kuhusu Kristo.

**KUJIFUNZA KWA MOYO**

Je, una hofu kwa sababu huna la kuwaambia wale unaotaka kuwashuhudia? Kuhisi hivyo ni kawaida. Ili kuwa na ujasiri zaidi:


1. Jifunze "mpango wa wokovu" katika *Maelezo ya ziada #6*
2. Jifunze mpango huu kwa moyo, pamoja na mistari ya Biblia.
3. Kata kurasa katika *Maelezo ya ziada* inayo-eleza juu ya mpango wa wokovu na kuliweka ndani ya Biblia yako.

**WIKI HII**

Utaanza kushuhudia lini?

Juma hili mshuhudie mtu mmoja aliye katika orodha yako kuhusu mpango wa wokovu. Usisubiri muda mwingi ukapita. Kama huna mstari uliokariri, basi unawe-za kuanza na Yohana 3:16.

Kama unataka kujua jinsi ya kutumia ushuhuda wako, angalia *Maelezo ya ziada #6* na utaona maelezo yatakayokusaidia kuwaambia wengine yale Kristo ameku-tendea katika maisha yako.



**KUWA IMARA**

**Soma Warumi 5-8**
(soma kila sura kwa siku mbili mfululizo ili uweze kuufahamu vyema).

**Kariri**

*Jifunze mpango wa wokovu katika Maelezo ya ziada # 6*

8. Nuru yako yaangaza kiasi gani? Kwa kufahamu kwamba wewe ni nuru ya ulimwengu, weka alama kando ya maelezo yanayofafanua maisha yako.



- ❏ Ninapenda kueleza habari za Kristo, kwa sababu amenibadilisha
- ❏ Wakati mwingine naangaza, laki wakati mwingine nuru yangu inafunikwa.
- ❏ Sijui jinsi ya kushuhudia juu ya Kristo.
- ❏ Naona haya kuzungumza kuhusu Kristo.
- ❏ Kufikia sasa nuru yangu imeangaza kidogo sana.

9. Tunapata kile tunachokiita Agano Kuu katika Mathayo 28:19-20. Katika agano hili Kristo anatuagiza tufanye nini? ______________________________

______________________________________________________________

**JINSI YA KUSHUHUDIA: MAMBO YA KUFANYA**

1. Mruhusu Kristo ayabadilishe maisha yako.Kumbuka kwamba maneno yako yatakosa maana kamili kama hayataambatana na tabia yako nzuri. Mathayo 5:16
2. Tumia Biblia. Ni neno la Mungu, na ni silaha yenye nguvu inayoyoon-doa kuchanganyikiwa kwa fahamu za wenye dhambi. Waebrania 4:12.
3. Mtegemee Roho Mtakatifu akusaidie katika kushuhudia. Yeye husa-dikisha ulimwengu juu ya dhambi akiwatayarisha kukusikiliza wakati unaposhuhudia habari za wokovu (Yohana16:8). Usimlazimishe mtu. Mungu mwenyewe atafanya kazi katika mioyo yao.
4. Ombea rafiki zako amboa hawajampokea Kristo bila kukoma. Tafuta muda wa kuwashuhudia.
5. Mhurumie asiyeamini ukielewa kwamba yeye ni mtumwa wa dhambi. Yeye si adui wako, bali ni mtumwa wa shetani.
6. Shuhudia kwa unyenyekevu (1Petro 3:15). Elewa kwamba kama si neema ya Mungu, basi ungalikuwa katika hali iyo hiyo.
7. Uwe na adabu. Hakikisha kwamba huyu mtu asiyeamini anakuelewa kwamba unataka kumsaidia. Usimhukumu.
8. Uwe mtu asili. Kumbuka watu muhimu ulio nao ni ndugu na rafiki zako. Usiogope kuwashuhudia. Tumia muda huu kwa faida.
9. Chukua baadhi ya vijikaratasi au vijitabu vya injili na uanze kuvigawa sasa. Muulize mchungaji wako au mzee wa kanisa jinsi ya kuvipata.
10. Uwe na ujasiri. Hata kama wote hawatapokea ujumbe wako, kumbuka kwamba wewe ni mhubiri wa habari njema iletayo uzima wa milele (Warumi 1:16). Tufahamu watu wengi wapo tayari kupokea kuliko tunavyodhania



## Hatua ya 11
# Ubatizo Na Ushirika Takatifu

Jibu KWELI (K) au SI KWELI (S)
_____ Ni lazima nibatizwe ili nipate kwenda Mbinguni.
_____ Ubatizo pamoja na chakula cha Bwana hunifanya kuwa mtakatifu zaidi.
_____ Mkate na kinywaji katika Chakula cha Bwana ni ishara ya damu na mwili wa Kristo.

**UBATIZO**

1. Yesu, kabla kupaa kwenda mbinguni, aliwaagiza wafuasi wake wafanye mataifa yote kuwa wanafunzi. Mtu anastahili kuchukua hatua gani ya kwanza anapofanyika kuwa mwanafunzi wa Kristo kwa mujibu wa Mathayo 28:19-20? ______________________________

   ***Ubatizo si chaguo, bali ni amri ambayo kila muumini hana budi kuitii.***

2. Si sharti kubatizwa ili kupata wokovu. Ubatizo ni tokeo la wokovu ambalo nimeupata tayari. Hebu tuangalie mfano wa towashi Mwethiopia katika Matendo 8:26-40. Soma kifungu chote. Kutokana na vigfungu vya 36 hadi 37, mtu anahitaji kutimiza masharti yapi ili kubatizwa?

   ______________________________

   Baada ya kumwamini Kristo, yule towashi alitaka kueleza watu kuhusu imani yake mpya. Aliweza kufanya hivyo namna gani? ___________

   ______________________________

   ***Tunaona kwamba ubatizo ni namna ya kudhihirishia watu kwa wazi wazi kwamba tumeokoka.***

3. Kutokana na Matendo 2:41, baada ya kulipokea neno, __________ na watu wapatao elfu tatu ___________kwa idadi yao.

   ***Wale watu elfu tatu, kwa kubatizwa, walijitambulisha na kanisa la Jerusalemu. Vivyo hivyo, tunapobatizwa tunajitambulisha na kanisa mahali tulipo.***

**Kuna watu ambao wana mawazo ya kupotosha kuhusu ubatizo. Basi ni muhimu kutambua kwamba:**

1. Ubatizo huwezi kutuokoa
2. Ubatizo sio hatua ya kuufikia wokovu
3. Ubatizo hautufanyi kuwa watakatifu sana, ijapokuwa hutuchochea kuishi maisha matakatifu.

**KUANGALIA KWA KINA**

Soma Warumi 6:1-4. Ukiangalia mstari huu kwa mara ya kwanza utadhani kwamba inaongea kuhusu kubatizwa kwa maji. Lakini neno "batizo" limetumika hapa kumaanisha kujitambulisha na Kristo.

Tunapompokea Kristo, tunafanywa kuwa moja naye katika kifo chake, kuzikwa kwake, na kufufuka kwake. Hivyo katika Kristo sisi ni watu wapya.

Ubatizo wa maji ni ishara ya mabadiliko hayo ambayo yalitokea wakati wa kuokoka. Kuchovywa ndani ya maji inaonyesha kuambatanishwa na Kristo katika kifo chake na kuzikwa kwake, na kwamba utu wetu wa kale "ulikufa". Kuibuka majini huonyesha kufufuka kwetu kwa maisha mapya.



**AMUA**

Ikiwa umempokea Kristo tayari, je umemtii kwa kubatizwa?

Ndiyo ❑ La ❑

Kama bado hujabatizwa, tafuta ushauri wa mchngaji au mzee wa kanisa lako leo.

**HEBU FIKIRI**

Watu wengine wana mawazo yaliyopotoka juu ya Meza ya Bwana. Hivyo ni muhimu kujua kwamba:


1. Ushirika huo (Chakula cha Bwana) si ushirikina.
2. Hakitufanyi kuwa watakatifu zaidi, bali kinatuchochea kuishi maisha matakatifu.
3. Kinywaji hicho hakiwezi kugeuka na kuwa damu ya Kristo, wala mkate kugeuka na kuwa mwili wa Kristo, bali ni ishara tu ya damu na mwili wa Kristo.

**KUKUMBUKA**

Kutokana na Waebrania 10:10-12, je Kristo anatoa mwili wake kwa mara ngapi kama dhabihu ya dhambi?

____________________ kwa wakati wote.

**KUWA IMARA**



**Soma Yakobo 1-5; Zaburi 19 na Zaburi 27** (sura moja kwa siku)

**Kariri Mathayo 28:19**

*"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na mwana, na Roho Mtakatifu".*

## MEZA YA BWANA

Ushirika wa meza ya Bwana ilianzishwa na Yesu usiku ule wa kusalitiwa kwake. Ushirika wa Meza ya Bwana ni takatifu na maalum sana, na si jambo la siri au ushirikina.

4. Tafadhali soma 1 Wakorintho 11:23-26. Kwa mujibu wa mstari wa 26:

   Tunatangaza nini? ____________________

   Hadi lini? ____________________

   Kifungu hiki kinatufundisha maana ya Meza Ya Bwana, kutukumbusha kujitoa kwa Kristo pale msalabani, na kuja kwake mara ya pili.

5. Je maana ya "fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu" ni nini? ________

   ____________________

6. Kutokana na mistari ya 24 na 25, maana ya mkate na kikombe cha divai ni nini?

   Mkate ____________________

   Kikombe cha divai ____________________

7. Sasa soma 1 Wakorintho 11:27-31. Kifungu cha 28 kinasema kwamba kabla mtu kula chakula cha Bwana ni lazima ajichunguze mwenyewe.

   Huku kujichunguza kuna maana gani kwako? ____________________

   ____________________

   ____________________

8. 1 Wakorintho 10:16-17 inasisitiza namna nyingine ya chakula cha Bwana, ambayo ni ushirika na umoja. Maana ya kuwa katika ushirika na waumini wengine ni nini? ____________________

   ____________________

   ____________________

**KWA MUHTASARI**

1. Meza ya Bwana ni ukumbusho wa dhabihu ya Kristo mpaka atakapokuja.
2. Ni tendo la utii na wakati wa kuwa na ushirika na Kristo na kaka na dada zetu katika imani.



# Hatua ya 12
# Jamaa

Jibu KWELI (K) au SI KWELI (S)

______ Kazi ya msingi ya mwanamume ni kumpenda mke wake.

______ Heshima ya mwanamke kwa mumewe inaweza kumleta mumewe kwa Kristo

______ Hata kama mmoja wa wazazi sio muumini, bado anahitaji kupendwa na mwenzake.

## JAMII YA KIKRISTO

Nyumba ya Mkristo ni kitovu cha msaada, ulinzi na kufundishana kwa wema. Hapo ndipo watoto hufundishwa jinsi ya kukabiliana na mambo mbalimbali katika maisha. Kristo asipokuwa kiongozi wa nyumba, basi nyumba hiyo inageuka kuwa uwanja wa vita na kuchanganyikiwa badala ya kuwa kimbilio.

### Mpango wa Mungu kwa jamii katika kitabu cha Mwanzo

*"Si vema kwa mtu huyu kukaa pekee yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye …" Mwanza 2:18*

- Mungu ndiye aliyemuumba Hawa kama mke wa Adamu. Kwa hivyo chanzo cha nyumba ni Mungu.
- Mke ananenwa kuwa msaidizi anayefaa na kumtosheleza mumewe. Wote kwa pamoja, mke na mume wanakamilishana. Kuungana kwao ni vyema kuliko wakiwa mtu pekee yake.

"*Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakua mwili mmoja, nao walikuwa uchi wote wawili, Adamu na mke wala hawakuona haya.*" Mwanzo 2:24-25

- Waliooana wanatakiwa kujitenga na wazazi wao, ili kuunda jamii yao. Hivi ndivyo watavyoweza kujifunza kutegemeana. Hakuna njia nyingine.
- "Mwili mmoja" ni kuishi kwa muungano kama marafiki wanaoshirikishana mawazo ya ndani bila kuwa na mashindano.
- Ngono katika ndoa si kitendo cha aibu, bali ni zawadi kutoka kwa Mungu kwa waliooana kwa wema wao. Watoto watakaozaliwa ni baraka kutoka kwa Mungu.

## JUKUMU LAKO NYUMBANI

1. Mungu anawaamuru waume namna gani katika vifungu vifuatavyo?

   Waefeso 5:25 ____________________________________________

   Wakolosai 3:19 __________________________________________

   1 Petero 3:7 ____________________________________________

   Je, mnatimiza hayo waume? Kama sivyo, basi unahitaji kubadilisha nini? Kristo alikuw ana upendo wa aina gani kwa kanisa lake? Hivyo ndivyo unavyohitajika kuishi katika upendo na mkeo.

**JADILI**

Biblia inanena kuhusu mwanamke kumtii mumewe. Je unaamini kwamba hii inampa mwanamume kuwa na haki ya kumdhulumu mkewe? Kwa nini sivyo?

______________________________

______________________________

**HEBU FIKIRI**

Kuna vitu vingi ambavyo vinaweza kuharibu umoja katika nyumba. Andika baadhi yao hapa chini:

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

**WIKI HII**



Moja kati ya vitisho katika umoja wa jamii ni kwamba hatujatilia maanani muda wa kuwa pamoja. Kuna nyakatika ambapo hawaoni upendo wetu ijapokuwa tunawapenda. Leo utafanya nini ili kudhibitisha upendo wako kwa mume wako au mke wako (au mmoja katika jamaa yako)?

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

Utafanya nini na watoto wako (au mmoja katika jamaa yako) ili kuonyesha kwamba unawapenda?

______________________________

______________________________

______________________________

**KUANGALIA KWA KINA**

Upendo ni muhimu sana katika jamii ya kikiristo. Katika 1 Wakorintho 13:4-7, Paulo anaelezea maana ya upendo wa kweli. Chukua karatasi halafu andika tabia za upendo zilizo-elezwa hapo au piga mistari maneno ambayo yana maana kwako.



**KUWA IMARA**

**Soma Wafilipi 1-4;**

**Zaburi 37, 51 na 139 (sura moja kwa siku).**

**Kariri Wafilipi 2:3-4**

***'Msitende neno lolote Kwa kushindana wala Kwa majivuno, bali Kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kulik o nafsi yake. Kila mtu na asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine.'***

2. Je Mungu amewapa wanawake amri gani?

   Waefeso 5:33 ____________________

   1 Petro 3:1-2____________________

3. Mungu anadai kitu gani kutoka kwa wanaume na wanawake katika Waefeso 6:4? (Vitu ambavyo hawastahili kufanya). ____________________

   ____________________

   Kwa mfano, wazazi wanaweza kuwachokoza au kuwaudhi watoto wao kwa kufanya nini?____________________

   ____________________

4. Kutokana na Kumbukumbu La Torati 6:6-7, ni kwa hali gani, na mahali gani panapofaa kwa kumfunza mtoto?____________________

   ____________________

   Washirikishe familia mambo uliyojifunza wakati wa faragha na Mungu. Soma Biblia na kuomba pamoja kuhusu mahitaji ya kila moja.

5. Je Mungu amewaagiza watoto wafanye nini kwa mujibu wa Waefeso 6:1-2 ____________________

6. Kuna sheria chache zinazoweza kuleta amani na umoja katika jamii. Zote zinawahusu wazazi na watoto. Je ni zipi hizo?

   Waefeso 5:21 ____________________

   ____________________

   Wafilipi 2:3-4 ____________________

   ____________________

## HALI ZISIZO ZA KAWAIDA

***Kama jamaa yako si Wakiristo***

Wapende. Ni muhimu kwamba usiwadharau wasioamini katika jamaa yako. Wanafanya dhambi kwa sababu hawajamtambua Kristo bado. Hata wewe ulikuwa hivyo wakati fulani. Kumbuka kwamba "tulipokuwa tungali wenye dhambi Kristo alikufa kwa ajili yetu" (Warumi 5:8). Onyesha upendo wako halisi kwa vitendo.

Waongoze kwa Kristo kwa ushuhuda wako mwema. *"…Kadhalika ninyi wake, watiini waume zenu; kusudi, ikiwa wako wasioamini Neno, wavutwe kwa mwenendo wa wake zao, pasipo lile neno; wakiutazamia mwenendo wenu safi, na wa hofu"* 1 Petero 3:1-2.


Hayo maneno yametumika kwa kuwashauri wanawake wa Kikristo, lakini yanaweza pia kutumika kwa Mkiristo yeyote aliye na watu wa jamaa yake ambao hawajaokoka. Ushuhuda wako ni muhimu kwa kubadilishwa kwa jamaa yako. Onyesha imani yako kwa matendo yako badala ya kuwakosoa na kuwalazimisha (Mathayo 5:16).

***Mkiishi pamoja bila kuoana***

Ijapokuwa ni kawaida katika jamii yetu kuwa na watu wanaoishi pamoja bila kuoana, Biblia inaita hii uzinzi. Je, wewe na mwenzio mna ndoa halali? Kama sivyo, basi rekebisha mara moja. Pata mashauri kutoka kwa mchungaji wako au mzee wa kanisa lako.

***Kama u peke yako***

Ukiwa peke yako, basi una changamoto ya kuishi kwa uadilifu sana, ukijiepusha na ngono nje ya ndoa. Jiweke nadhifu kwa atakayekuoa au utakayeolewa naye. Mungu anakutakia mema. Kama hujajiweka nadhifu, basi mwombe Mungu akusamehe dhambi zako na kukufanya kuishi katika utakatifu. Utahitaji msaada wa Mkristo aliyekomaa au mchungaji.




# Hatua ya 13
# Kumfuata Yesu

Jibu KWELI (K) au SI KWELI (S)
____ Mkristo anahusika sana katika kukua kwake kiroho.
____ Kuwa na ushirika na mwili wa Kristo si muhimu.
____ Inawezekana kuwa na ushirika wa kufana kila wakati na Mungu.

**TABIA ZA MISINGI KATIKA KUENDELEZA MAISHA YAKO**

Umechukua hatua za muhimu katika kutembea na Kristo katika masomo yaliyopita.

Angalia tabia chache katika picha hizi zinazoambatana na maisha ya Mkristo.


____________________




____________________


____________________


____________________


____________________


____________________

**Tabia hizi za misingi ni za maana katika kukua kwako. Usiyapuuze kamwe.**

Ni muhimu kuyamudu maisha yako ukitoa muda wako kwa mambo yaliyo muhimu. Hii inaitwa kuzingatia mambo muhimu. Katika Yohana 17:1-26, Yesu Kristo alizungumza juu ya mambo matatu ambayo ni muhimu katika maisha ya Mkristo, yaani:

- Kujitoa kwa ajili ya Kristo
- Kujitoa kwa ajili ya waumini wengine
- Kujitoa kwa ajili ya kazi ya Kristo hapa duniani.

1. Kristo anataka kuwa na uhusiano gani nawe?
   Yohana 17:3 ____________________
   Yohana 17:13 ____________________
2. Yohana 17:11, inaeleza ushirika ambao Yesu anataka kuwe baina ya Wakristo.
   "Kwa jina lako ulilonipa uwalinde hawa, ili ____________________, kama sisi tulivyo."
3. Yohana 17:23, "Wawe wamekamilika katika umoja ili ulimwengu upate kujua ________________, na ______________________________kama ulivyonipenda mimi."

   Upendo na umoja miongoni mwa Wakristo ni ushuhuda wenye nguvu sana unayofanya ujumbe wetu kuwa halisi. Yohana 14:34-35.

**ANGALIA**

Je, unatumia mpangilio uliyopewa katika somo la 8 kwa ibada zako?

Ndiyo ❏ La ❏

Umetenga muda gani ili kukutana na Mungu kila siku?

______________________

Utakuza uhusiano wako na wakristo wengine vipi?

______________________
______________________
______________________
______________________

Utaonyesha ulimwengu vipi kwamba Kristo anaishi ndani yako?


______________________
______________________
______________________
______________________

**KUANGALIA KWA KINA**
Soma Yohana 15:16. Yesu anatamani kwamba walio wake wazae matunda ya kudumu kwa wingi. Kuna namna mbili ya matunda.

Hizi matunda ni zipi kwa mujibu wa Wagalatia 5:22-23 na Mathayo 28:18-20?

______________________
______________________
______________________

**KUWA IMARA**



**Soma**
**1 Wathesalonike 1- 5**
**na 2 Thesalonike 1-3**
(sura moja kwa siku).

**Kariri Mithali 3:5-6**

*"Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe; Katika njia zako zote mkiri yeye, Naye atayanyosha mapito yako."*

**KUTEMBERA KATIKA IMANI**

4. Paulo anasema kwamba "tunaishi kwa imani, walio sio kwa kuona." (2 Wakorintho 5:7). Imani immelezwa vipi katika Waebrania 11:1?

______________________________________________

______________________________________________

5. Waebrania 11:6 inasema kwamba "Bila imani ni vigumu kumpendeza Mungu, kwa maana kila amjiaye lazima awe na imani kwamba ____________________na kwamba ____________________ wanaomtafuta kwa thati.

6. Hebu fikiri nini maana ya "kutembea kwa imani", alafu tafakari kuhusu maneno yaliyo ndani ya mraba ulio hapa chini.

> *Imani si tumaini lililo na upofu, bali ni kuwa na bayana kwamba Mungu ni mwaminifu na kwamba atatenda yote aliyoahidi. Kuwa na imani kwa Mungu inamaanisha kutotegemea uwezo wetu wenyewe, bali kutegemea uwezo wa Mungu tu.*
>
> *Kutembea katika imani ni kutenda kila siku yale Bwana anakufundisha. Hi ndiyo sababu ni muhimu kudumisha na kutunza ushirika wako wa ndani na Mungu.*

7. Yesu ameeleza vipi uhusiano wake na wafuasi wake katika Yohana 15:4-5? ______________________________________

______________________________________________

Uhusiano wetu na Mungu unafananishwa na mzabibu, Kristo akiwa ndiye mzabibu nasi tukiwa ni matawi.

8. Mbona ni muhimu kudumisha uhusiano huo na Kristo? ____________

______________________________________________

9. Unafikiri Yesu alimaanisha nini kwa maneno "dumu ndani yangu" (kifungu cha 4).______________________________________

10. Kwa mujibu wa Yohana 15:10, utawezaje kudumu katika upendo wake?

______________________________________________

**KUJITOLEA KWAKO**

11. Soma maneno ya Yesu katika Luka 9:23. Je, unahitaji kumfuata?
Ndiyo ❏ La ❏

12. Je, u tayari kuacha tamaa zako ili ufuate kwa furaha matakwa ya Kristo kwa maisha yako? Ndiyo ❏ La ❏

- Endelea kufuata kielelezo na tabia aulizojufunza
- Tenda yale Mungu anakuonyesha kila siku
- Tunza uhusiano wako na Mungu

## Kiambatisho cha 1

Pasua kurasa hili kenye alama ya mistari. Unaweza kuukunja na kuuweka kwa Biblia yako

***Wagalatia 2:20*** — ***Hatua ya 4***

***Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu".***

***Yoshua 1:8*** — ***Hatua ya 8***

***"Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawa sawa na maneno yote yaliyoandikwa humo; maana ndipo utakapoifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapositawi sana"***

***Mithali 3:5-6*** — ***Hatua ya 13***

***"Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe; Katika njia zako zote mkiri yeye, Naye atayanyosha mapito yako.***

***1 Yahana1:9*** — ***Hatua ya 3***

***"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote".***

***Wafilipi 4:6-7*** — ***Hatua ya 7***

***"Msijisumbue kwa jambo lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru., haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu."***

***Wafilipi 2:3-4*** — ***Hatua ya 12***

***'Msitende neno lolote Kwa kushindana wala Kwa majivuno, bali Kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake. Kila mtu na asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine.***

***Yohana 10:27-28*** — ***Hatua ya 2***

***"Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata. Nami nawapa uzima wa milele; wala hawata potea kamwe wala hakuna mtu atakaye wapokonya katika mikono yangu".***

***2 Timotheo3:16 –17*** — ***Hatua ya 6***

***"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema."***

***Mathayo 28:19*** — ***Hatua ya 10-11***

***"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na mwana, na Roho Mtakatifu".***

***Waefeso 2:8-9*** — ***Hatua ya 1***

***"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu"***

***1 Wakorintho 12:13*** — ***Hatua ya 5***

***"Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani,ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja".***

***Waebrania 10:24-25*** — ***Hatua ya 9***

***"Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kua inakaribia."***

# Kiambatisho cha 2

Pasua kurasa hili kenye alama ya mistari. Unaweza kuukunja na kuuweka kwa Biblia yako

## MIMI NI NANI KATIKA KRISTO?

Mimi ni kiumbe kipya (2 Kor. 5:17)
Mimi ni mtoto wa Mungu (Yoh. 1:12; Rumi 8:14; Galatia 3:26; 4:6)
Nimekombolewa na kusamehewa dhambi zangu zote (Kolosai 1:14)
Mimi niko huru milele mbali na hukumu. (Rumi 8:1)
Nimewekwa huru mbali na nguvu ya dhambi (Rumi 6:1-6)
Ninayo haki ya kwenda mbele za Mungu bila aibu, kutafuta rehema mbele ya kiti cha enzi cha Mungu wakati wa mahitaji. (Waebr. 4:12)
Nina haki katika Kristo, nimesamehewa kabisa. (Rumi 5:1)
Mimi ni mtumwa wa haki. (Rumi 6:18)
Mimi ni mtakatifu. (Efeso 1:1; 1 Kor. 1:2; Flp 1:1)
Mimi ni chumvi ya dunia. (Mat. 5:1)
Mimi ni nuru ya ulimwengu, na mtu wa kweli. (Mat. 5:14)
Mimi ni rafiki yake Kristo. (Yoh. 15:15)
Mimi nimechaguliwa na Kristo kumzalia matunda. (Yoh. 15:16)
Nimefanyika kuwa mtumishi wa Mungu. (Rumi 6:22;Efeso 3:1; 4:1)
Mimi ni hekalu, makao ya Roho mtakatifu. (1Kor. 3:16; 6:19)
Nimenunuliwa kwa bei, na sasa mimi ni mali ya Mungu, siyo mimi tena, bali Kristo anaishi ndani yangu. (1Kor. 6:19-20; 2Kor. 5:14-15)
Mimi ni mshirika wa mwili wa Kristo. (1 Kor. 12:27 Efeso 5:30)
Nimepatanishwa na Mungu. Mimi ni mpatanishi. (2 Kor. 5:18-19)
Nilisulubiwa pamoja na Kristo, si mimi ninayeishi, bali Kristo ndani yangu. (Gal. 2:20)
Nilichaguliwa na Kristo kabla ya kuwekwa kwa misingi ya ulimwengu kuwa mtakatifu, bila mawaa, mbele zake. (Efeso 1:4)
Mimi ni mrithi wa Mungu kwa sababu, ni mtoto wake. (Gal. 4:6-7)
Mimi ni mtenda kazi pamoja na Mungu, nimezaliwa mara ya pili kwa ajili ya kazi yake. (Efeso 2:10)
Mimi ni mtakatifu na mwenye haki. (Efeso 4:24)
Mimi ni raia wa Mbinguni. (Flp 6:20; Efeso 2:6)
Mimi ni mpitaji katika ulimwengu huu, ambamo ninaishi kwa muda tu. (1Pet. 2:11)
Mimi ni mtoto wa nuru, na sio wa giza. (1Thes. 5:5)
Nimekwisha kutolewa kutoka kwenye ufalme wa shetani na kuingizwa katika ufalme wa Mungu. (Kolosai 1:13)
Mimi ni adui wa yule mwovu. (1Pet. 2:8)
Mimi nimezaliwa na Mungu. Shetani hana amri ya kunigusa. (1Yoh. 5:18)
Kristo anaishi ndani yangu. (Kolosai 1:27)
Mimi nimechaguliwa na Mungu, aliye Mtakatifu na mwenye upendo. (Kolosai 3:13; 1Thes.1:4)
Nimepokea ahadi kubwa sana na za thamani sana. (2Pet. 1:4)
Nitakuwa kama Kristo atakaporudi. (1Yoh. 3:1-2)
Kwa neema ya Mungu nipo kama nilivyo. (1Kolosai15:10)

Adapted from Victory Over the Darkness by Neil T. Anderson

## JE NAWEZAJE KUUNGAMA DHAMBI ZANGU?

"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote". 1 Yahana1:9

Kuungama ni zaidi ya kusema, "nilitenda dhambi." Ungamano la kweli linahitaji mambo haya:

a. Unyofu.
b. Kutubu kwa kusikitika na kutotamani kurudia dhambi tena.
c. Kumtajia Mungu dhambi niliyotenda.
d. Kuwa mwepesi wa kutambua makosa yangu. Nahitaji kutubu mara tu ninapotambua kwamba nimefanya dhambi. Nisipofanya hivyo, basi kuna hatari ya kufanya dhambi zaidi.
e. Kunyenyekea na kuomba walioathiriwa na dhambi zangu msamaha.
f. Kupokea msamaha. Hatuhitaji kuendelea kujilaumu kwa dhambi ambazo tumetubu tayari. Ni sharti tupokee msamaha wa Mungu, tukimwamini na kumshukuru. Tukatae shutuma za Shetani kwamba hatuwezi kusamehewa.

## Kiambatisho cha 3

Pasua kurasa hili kenye alama ya mistari. Unaweza kuukunja na kuuweka kwa Biblia yako

### HALI ISHIRINI ZA MAFANIKIO

Mtu moja alisema kwamba mafanikio huja kwa "kuweza," na kushindwa huja kwa "kutokuweza." Kuamini kuwa unaweza kufanikiwa kukua na kukomaa hakuhitaji bidii kuliko kutoamini kuwa huwezi kufanikiwa. Basi, mbona usiamini kuwa *unaweza* kutembea katika imani na Roho, kuyashinda majaribu ya ulimwengu huu, shetani, na mwili, na kwamba unaweza kukua na kukomaa kama Mkristo.

1. Mbona nisema kwamba siwezi wakati ambapo Biblia inasema kwamba nayaweza mambo yote kwa Kristo anitiaye nguvu (Wafilipi 4:13)?
2. Mbona niwe na upungufu ninapofahamu kwamba Mungu atakutana na mahitaji yangu kwa kadiri ya utajiri wake katika utukufu ndani ya Kristo Yesu (Wafilipi 4:19)?
3. Mbona niwe na hofu wakati ambapo Mungu anasema kwamba hakunipa roho ya woga, bali ya nguvu, ya upendo, na moyo wa kiasi (2 Timotheo 1:7)?
4. Mbona nikose imani ya kutimiza mwito wangu nikifahamu vyema kwamba Mungu amenipa kipimo cha imani (Warumi 12:3)?
5. Mbona niwe dhaifu wakati ambapo Biblia inasema kwamba Mungu ndiye nguvu katika maisha yangu na kwamba nitadhihirisha uwezo na kufanya jambo kwa kuwa namjua Mungu (Zaburi 27:1; Danieli 11:32)?
6. Mboni nimruhusu Shetani kutawala maisha yangu wakati ambapo yeye aliye ndani yangu ni mkuu kuliko yeye aliye ulimwenguni (1 Yohana 4:4)?
7. Mbona nikubali kushindwa wakati Biblia inasema kwamba Mungu huniongoza kwa ushindi (2 Wakorintho 2:14)?
8. Mbona nikose hekima wakati ambapo Kristo alikuwa hekima kwa ajili yangu kutoka kwa Mungu na Mungu hunipa hekima kwa wingi ninapomuomba kunipa hiyo hekima (1 Wakorintho 1:30; Yakobo 1:5)?
9. Mbona nihuzunike wakati ambapo naweza kukumbuka fadhili, huruma na uaminifu wa Mungu na kuwa na tumaini (Maombolezo 3:21-23)?
10. Mbona niwe na hofu na kuhuzunika wakati ambapo naweza kumtwika Kristo hofu zangu zote kwa Kristo ambaye ananijali (1 Petero 5:7)?
11. Mbona niwe mfungwa wakati ambapo natambua kwamba kuna huru mahali ambapo roho wa Bwana yupo (Wagalatia 5:1)?
12. Mbona nihisi kuhukumiwa wakati ambapo Biblia inasema kwamba sihukumiwi kwa kuwa nimo ndani ya Kristo Yesu (Warumi 8:1)?
13. Mbona nihisi kuwa pweke wakati ambapo Yesu alisema kwamba yuko nami nyakati zote na kwamba hawezi kuniacha au kunitupa (Mathay 28:20; Waebrania 13:5)?
14. Mbona nihisi kuwa nimelaaniwa au nina bahati mbaya wakati ambapo Biblia inasema kwamba Kristo alinikomboa kutokana na laana ya torati ili niweze kupokea Roho Wake (Wagalatia 3:13-14)?
15. Mbona nisitosheke wakati ambapo mimi, kama Paulo, naweza kujifunza kutosheka kwa hali zote (Wafilipi 4:11)?
16. Mbona nihisi kwamba sifai wakati ambapo Kristo amekuwa dhambi kwa ajili yangu ili niwe haki ya Mungu ndani yake (2 Wakorintho 5:21?
17. Mbona nione kwamba nadhulumiwa nikijua kwamba Mungu akiwa upande wangu, ni nani atakayenipinga (Warumu 8:31)?
18. Mbona nichanganyikiwe wakati ambapo Mungu ndiye mwanzilishi wa amani na kwamba yeye hunipa elimu kupitia kwa Roho Wake anayeishi ndani yangu (1 Wakorintho 2:12, 14:33)\?
19. Mbona nihisi kushindwa wakati ambapo mimi ni mshindi kwa mambo yote kupitia kwa Kristo (Warumi 8:37)?
20. Mbona nisongwe na mambo ya dunia wakati ambapo naweza kuwa jasiri nikifahamu kwamba Yesu ameshinda ulimwengu na mateso yake tayari (Yohana 16:33)?

Maneno haya yamenukuliwa kutoka kwa Ushindi Dhidi ya Giza
na Neil Anderson, uk. 115-117

# Kiambatisho cha 4

Pasua kurasa hili kenye alama ya mistari.  Unaweza kuukunja na kuuweka kwa Biblia yako

## MPANGILIO RAHISI KWA IBADA YAKO YA FARAGHA

**Tayarisha moyo wako**

- Jichunguze
- Tubu dhambi zako
- Ombea ufahamu

**Chunguza Biblia**

- KITU GANI kilichokupendeza sana?
- Wazo muhimu ni lipi?
- Linamaanisha nini kwako?

**Mwombe Bwana**

- ONGEA na Mungu kuhusu somo ambalo umesoma
- Mwabudu Bwana kwa jinsi alivyo
- Mshukuru Mungu kwa yale ametenda
- MWOMBE Mungu ukitumia orodha ya mahitaji uliyotayarisha

**Mwimbie Bwana**

Imba tenzi au nyimbo za kumsifu Mungu.  Hii itainua moyo wako na kukusaidi kumsifu Mungu.

**Weka katika vitendo mambo ambayo umejifunza**

Utafanya nini leo ili kuweka katika vitendo maishani mwako yale uliyojifunza?

**Tafakari na Kukariri**

Kwa mujibu wa vifungu ulivyosoma, tafuta kifungu kimoja cha kutafakari na kukariri.  Andika kifungu hicho katika daftari au katika karatasi nene (card) chenye kipimo cha 3 x 5.  Beba hii karatasi uendapo ili uweze kukariri kifungu hicho.

## KUTAYARISHA MOYO WAKO

Bwana, asubuhi utaisikia sauti yangu, Asubuhi nitakupangia dua yangu na kutazamia (Zaburi 5:3).

Ee Mungu, unichunguze, uujue moyo wangu, Unijaribu, uyajue mawazo yangu; Uone kama iko njia iletayo majuto ndani yangu, Ukaniongoze katika njia ya milele (Zaburi 139:23-24).

Ee Mumngu, uniumbie moyo safi, Uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu ( Zaburi 51:10).

Nitajifurahisha sana kwa amri zako, Sitalisahau neno lako (Zaburi 119:18).

Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji (Waebrania 4:16)

## JINSI YA KUJIFUNZA BIBLIA

Somo: ____________________

Wazo la somo hili ni lipi? ____________________

____________________

Lina maana gani kwa  maisha yako? ____________________

____________________

Weka maswali haya muhimu katika akili kwa sababu yanaweza kukusaidia zaidi katika kujifunza kutoka kwa somo:

Je, kuna amri ya kutii?
Je, kuna mfano wa kufuata?
Je, kuna dhambi ya kutubu?
Je, kuna ahadi ya kudai?

## Kiambatisho cha 5

Pasua kurasa hili kenye alama ya mistari.  Unaweza kuukunja na kuuweka kwa Biblia yako

### TARATIBU RAHISI YA KUSOMA BIBLIA KWA MWAKA MOJA

| Sura | |
|---|---|
| YOHANA | 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 |
| MATENDO | 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 |
| 1 YOHANA | 1 2 3 4 5 |
| WARUMI | 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 |
| YAKOBO | 1 2 3 4 5 |
| WAFILIPI | 1 2 3 4 |
| 1 THESALONIKE | 1 2 3 4 5 |
| 2 THESALONIKE | 1 2 3 |
| ZABURI | 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 |
| WAEFESO | 1 2 3 4 5 6 |
| WAKOLOSAI | 1 2 3 4 |
| ZABURI | 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 |
| MATHAYO | 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 |
| ZABURI | 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 |
| 1 WAKORINTHO | 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 |
| 2 WAKORINTO | 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 |
| ZABURI | 31 32 33 34 35 36 37 38 39 40 |
| WAGALATIA | 1 2 3 4 5 6 |
| 1 TIMOTHEO | 1 2 3 4 5 6 |
| 2 TIMOTHEO | 1 2 3 4 |
| MARKO | 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 |
| ZABURI | 41 42 43 44 45 46 47 48 49 50 |
| TITO | 1 2 3 |
| FILEMONI | 1 |
| MWANZO | 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31 32 33 34 35 36 37 38 39 40 41 42 43 44 45 46 47 48 49 50 |
| ZABURI | 51 52 53 54 55 56 57 58 59 60 |
| 1 PETERO | 1 2 3 4 5 |
| 2 PETERO | 1 2 3 |
| UFUNUO | 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 |
| ZABURI | 61 62 63 64 65 66 67 68 69 70 |
| LUKA | 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 |

# Kiambatisho cha 6

Pasua kurasa hili kenye alama ya mistari.  Unaweza kuukunja na kuuweka kwa Biblia yako

## JINSI YA KUTAYARISHA USHUHUDA WAKO

Je, umewahi kufikiri unavyoweza kumweleza rafiki yako kuhusu imani yako?  Labda njia moja mwafaka ni kueleza kisa chako, au ushuhuda wako. Maelezo haya yatakusaidia kupanga mawazo yako na kutayarisha ushuhuda ulio rahisi na yenye nguvu.  Iandike kwa karatasi ili uweze kujifunza.  Unaweza kuifupisha (dakika 3), au kuirefusha.

### Mwongozo Katika kutayarisha Ushuhuda wako

1. "Kabla kumpokea Kristo…"  Uliishi na kuwa na mawazo aina gani kabla kumpokea Kristo?  Andika kwa muhtasari vitu vizuri na vitu vibaya katika maisha yako ulipokuwa bila Kristo.  Kisa chako kiwe cha kusisimua, ukieleza kuhusu ndoto zako,hisia zako, nia, tabia, mazoea na kadhalika.  Eleza ukweli bila kuongezea.
2. "Nilivyompokea Kristo…"  Fikiri kuongeza vitu hivi:  Ulimpokea Kristo vipi?  Wapi?  Uliomba vipi?  Ulihisi namna gani?  Mungu alikugusa namna gani?  Unaweza kutumia andiko ambalo lilikusaidia kuelewa injili.  Wasaidie watu kuielewa injili kutokana na ushuhuda wako.
3. "Baada ya kumpoke Kristo…"  Mambo gani yamefanyika tangu ulipompokea Kristo?  Eleza kinaganaga mabadiliko ambayo umeyapata tangu wakati huo.

### Mapendekezo

1. Rahisisha ushuhuda wako.  Tumia maneno ya kawaida.  Usitumie maneno ya "kidini."  Yawe maneno ambayo kila moja anaelewa. Epuka mambo yasiyofaa lakini ueleze kwa jinsi ya kusisimua.
2. Ushuhuda wako uwe kawaida tu (kama mazungumuzo).  Usihubiri. Onyesha furaha ili kufanya watu kustarehe.
3. Ushuhuda wako uwe wa kuvutia.  Tumia mifano inayovutia watu. Eleza kwa kutumia michoro panapohitajika kufanya hivyo ili msikilizaji wako aweze kuwa na picha katika fahamu zake kuhusu mambo unayosema.

## MPANGO WA WOKOVU

Kuna jinsi nyingi za kusimulia injili. Tunaweza kutumia moja wapo kati ya jinsi hizo lakini kuna mambo ya misingi ambayo mtu anahitaji kufahamu ili kuokolewa.  Mpangilio huu wa wokovu imetokana na "*Kanuni Nne Za Kiroho*."

1. *Mungu anakupenda na ana mpango mzuri kwa maisha yako*

Yohana 3:16 — Upendo wa Mungu
Yohana 10:10b — Mpango wa Mungu kwa maisha yako

2. *Mwanadamu ni mwenye dhambi na ametengwa na Mungu*

Warumi 3:23 — Sote tumefanya dhambi
Warumi 6:23 — Matukio ya dhambi ni kifo cha kiroho, kutengana na Mungu.
Waefeso 2:8-9 — Hatuwezi kujiokoa wenyewe

3. *Kristo Ndiye toleo la wokovu wetu.  Alikufa kwa ajili yetu na akafufuka*

Warumi 5:8 — Kristo alikufa kwa niaba yetu
Yohana 14:6 — Kristo ndiye njia ya pekee
1 Wakorintho 15:3-6 — Kristo alifufuka

4. *Ni lazima tumpokee Kristo kama Mwokozi wetu*

Yohana 1:12 — Mpokee Kristo ili uwe mwana wa Mungu
Ufunua 3:20 — Kristo anakungojea umkaribishe
Warumi 10:9 — Kwa imani umkaribishe maishani mwako.

# Cheti

Cheti hiki kimetunukiwa kwa

________________________________________

ambaye amekamilisha kwa kufaulu masomo yote katika kitabu hiki

## Maisha Mapya Ndani Ya Kristo Toleo la 1

### Hatua za msingi katika maisha ya Mkristo

*Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena,*
*bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili,*
*ninao katika imani ya mwana wa Mungu, ambaye alinipenda,*
*akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu". Wagalatia 2:20*

________________________________
Mwalimu

________________________
Tarehe



# NEW LIFE IN CHRIST

**Volume 1**

---

**Basic steps of the Christian life**